JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
MKOA WA SIMUYU

# MWONGOZO WA UWEKEZAJI MKOANI SIMIYU




2017

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**MKOA WA SIMUYU**

# MWONGOZO WA UWEKEZAJI MKOANI SIMIYU

2017

Mwongozo huu umefadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Kuandaliwa na Taasisi ya Tafiti za Kiuchumi na Kijamii (ESRF)

ISBN: 978 - 9987 - 770 - 28 - 1

# YALIYOMO


Utangulizi ........ iii

**Sehemu ya Kwanza: Kwa nini uwekeze Simiyu, Tanzania ........ 1**

1.1 Muhtasari wa sababu muhimu za kwa nini uwekeze Tanzania kwa jumla na hasa katika mkoa wa Simiyu ........ 1
1.1.1 Kwa nini uwekeze Tanzania? ........ 1
1.1.2 Sababu za kuwekeza Mkoa wa Simiyu? ........ 2

**Sehemu ya Pili: Hali ya kijamii na kiuchumi ya mkoa wa Simiyu ........ 5**

2.1 Eneo, idadi ya watu na hali ya hewa ........ 5
2.1 Kanda za ekolojia ya kilimo ........ 5

**Sehemu ya Tatu: Fursa za uwekezaji za kipaumbele mkoani Simiyu .. 7**

3.1 Fursa kuu za uwekezaji wa kimkakati katika Mkoa wa Simiyu ........ 7
3.2 Fursa mahsusi za uwekezaji mkoani Simiyu ........ 11
3.3 Makundi yanayolengwa na Mwongozo huu ........ 36

**Sehemu ya Nne: Uwezeshaji, Michakato, Mahitaji na Motisha ........ 37**

4.1 Uwezeshaji ........ 37
4.2 Michakato na Mahitaji ........ 39
4.3 Motisha ........ 41
4.4 Ujumuishaji na ushiriki wa sekta binafsi ........ 44

# UTANGULIZI

Karibu Mkoa wa Simiyu. Mwongozo wa Uwekezaji wa mkoa wa Simiyu umeandaliwa sambamba na sera ya uwekezaji ya Tanzania. Unaainisha fursa za uwekezaji zinazopatikana katika mkoa wa Simiyu. Vile vile unaendana na dira ya mkoa wa Simiyu kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano Dr. John Pombe Magufuli wa Tanzania mnamo tarehe 11, Januari 2017, na umeandaliwa kulingana na mifumo ya kimaendeleo ya kitaifa kama vile Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016-2021 *(FYDP II)*.

Mwongozo huu wa uwekezaji unatoa taarifa za uwekezaji kwa makampuni ya uwekezaji ya hapa nchini, ya nchi za nje na watu binafsi. Vile vile, Mwongozo unaainisha rasilimali na kubainisha fursa za uwekezaji zilizopo katika mkoa wa Simiyu ili kuchochea biashara, maendeleo na ukuaji wa uchumi. Pia Mwongozo unadhamiria kukuza uwezo wa ushindani wa Mkoa wa Simiyu katika maeneo ambayo Mkoa una fursa za kiuchumi. Madhumuni mengine ni kukuza uwezo wa uzalishaji katika sekta muhimu za msingi ili kuleta maendeleo endelevu yatakayochangia kukua kwa pato la jumla la Taifa na ustawi wa mkoa wa Simiyu.

Kwa hiyo, mkoa wa Simiyu na wilaya zake na Serikali za Mitaa: Bariadi, Busega, Itilima, Maswa, na Meatu wamedhamiria kutoa kipaumbele katika uwekezaji na kutoa huduma stahiki na motisha za kuvutia kwa wawekezaji katika Mkoa. Zaidi ya hayo, Ofisi ya Mkoa wa Simiyu na mamlaka zake za Serikali za Mitaa wataandaa mipango mwafaka na mazingira bora ya uendeshaji na ya kibiashara na watakuwa wanapatikana wakati wote ili kutoa maelezo zaidi kuhusu fursa zilizopo kwa wawekezaji wenye nia ya kuweka.

Napenda kulipongeza Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kwa msaada wa kifedha na utaalamu, pia Taasisi ya Utafiti wa Kiuchumi na Kijamii (ESRF) kwa kuandaa Mwongozo huu. Napenda pia, kuwashukuru

wataalamu waliochangia katika kuandaa Mwongozo huu; Dkt. Gratian Bamwenda, Dkt. Oswald Mashindano, Bibi Margareth Nzuki, Bwana Abdallah K. Hassan, na kupitiwa na Prof. Haidari Amani na Bwana Amon Manyama.

Mwisho, napenda kutumia fursa hii kuwakaribisha watu wote na makampuni kuja kuwekeza Simiyu, na kuwahakikishia huduma bora wakati wowote kutoka Ofisi ya Mkoa wa Simiyu ili kuufanya uwekezaji wenu uwe wa tija na wenye kukua kwa maslahi yetu sote.

Mheshimiwa Anthony Mtaka
Mkuu Wa Mkoa,
Simiyu, Tanzania

## SEHEMU YA KWANZA:

# KWA NINI UWEKEZE SIMIYU, TANZANIA

## 1.1 Muhtasari wa sababu muhimu za kuwekeza katika mkoa wa Simiyu nchini Tanzania

Simiyu ni sehemu ya Tanzania na fursa zake za uwekezaji zinahusiana na mazingira ya uwekezaji ya jumla ya kitaifa, sera pamoja na mifumo ya kiuchumi.

### *1.1.1 Kwa nini uwekeze Tanzania?*

Tanzania ina rasilimali nyingi za asili ambazo zinatoa fursa kadhaa za kuwekeza. Rasilimali hizo ni pamoja na eneo zuri sana la kijiografia, ambalo linafanya nchi sita zisizokuwa karibu na bahari *(Land locked)* kutegemea bandari za Tanzania kama njia rahisi za kuingizia na kutolea bidhaa zao; ardhi nzuri yenye rutuba; vivutio vingi maarufu vya kitalii, kama vile, mbuga ya taifa ya Serengeti, Mlima Kilimanjaro, bonde la Ngorongoro, na visiwa vya karafuu vya Zanzibar. Vitu vingine ni; rasilimali za asili kama vile madini; soko la kutosha la hapa nchini na la kikanda; vyanzo vya malighafi; stadi za aina nyingi, uhakika wa nguvu kazi kwa gharama nafuu; usalama wa mali; watu wachangamfu na rafiki.

Sababu zingine za kuwekeza Tanzania ni kama zifuatavyo:

- Usalama wa hali ya juu wa rasilimali zilizowekezwa kwa sababu ya utulivu mkubwa wa kisiasa usiokuwa na migogoro na migawanyiko ya kikabila; utawala wa kidemokrasia unaoheshimu maoni tofauti na utamaduni madhubuti wa kuheshimu katiba na utawala wa sheria;
- Utulivu wa uchumi mkubwa ulio rafiki kwa biashara na kiasi cha chini cha mfumko wa bei (kiasi cha 5%); viwango tulivu vya ubadilishaji

wa fedha vikiongezewa nguvu na uhaulishaji wa faida usiokuwa na vikwazo au masharti, ulipaji wa mikopo, mishahara, mirabaha na ada;

- Urasimu uliopunguzwa kwa kutumia huduma inayotolewa na Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania, ambacho ni wakala wa serikali *(One-stop center)* kinachowahudumia wawekezaji na biashara zilizosajiliwa;
- Hatua za ufanisi za kujenga uchumi wa soko huria zinazopongezwa na Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Dunia huku sheria za kusaidia biashara zikiboreshwa mara kwa mara kwa kupitia majadiliano thabiti kati ya serikali na sekta binafsi;
- Vivutio vya kunufaisha pande zote mbili kwa wawekezaji na maslahi ya ziada yaliyokubalika kwa wawekezaji wa kimkakati;
- Kukubalika kwa haraka kuwa ni sehemu nzuri ya kuingilia na kutokea kwa biashara zinazoingia Mashariki, Kusini na Afrika ya Kati;
- Fursa za kuvutia za kuwekeza katika miundombinu na kuendeleza rasilimali watu;
- Uhakika wa uwekezaji unachangiwa na usuluhishi wa migogoro; rasilimali zilizowekezwa nchini Tanzania hulindwa dhidi ya machafuko ya kisiasa, utaifishwaji na unyang'anyi;
- Kampuni yoyote ya nje inayofanya shughuli zake Tanzania inaweza kupata mkopo kutoka taasisi za kifedha za hapa nchini hadi kiwango kilichowekwa na Benki Kuu ya Tanzania. Benki kubwa kama vile Standard Chartered, ABSA, Barclays, Citibank, Stanbic, Exim zimewekeza nchini Tanzania;

### *1.1.2 Sababu za kuwekeza Mkoa wa Simiyu*

Simiyu ni miongoni mwa mikoa mipya hapa nchini. Mkoa wa Simiyu una eneo la kilomita za mraba 23,807.7 ambazo ni sawa na hekta 23,807,700. Mkoa huu unatimiza miaka mitano mwaka huu wa 2017 tangu ulipoanzishwa mwaka 2012. Kwa maneno mengine Simiyu bado ni mkoa mpya kati ya mikoa 30 ya kiutawala nchini, kwa hiyo unahitaji kutazamwa kwa namna ya kipekee katika biashara na uwekezaji. Mkoa wa Simiyu unaunganishwa kwa urahisi na nchi za Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda, na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Zifuatazo ni miomgoni mwa sababu za kuwekeza Mkoa wa Simiyu

- Mkoa huu unafaa kwa uwekezaji kwa sababu ya hali nzuri ya hewa, ambayo ni nzuri kwa utalii, kilimo na ufugaji. Amani na utulivu wa kisiasa ambavyo hujenga mazingira ya usalama pamoja na kiwango cha chini cha uhalifu ni vivutio vingine vya kumfanya mtu awekeze katika mkoa huu. Wawekezaji hawana haja ya kuwa na wasiwasi kuhusu usalama wa mali zao watakazowekeza katika mkoa huu. Zaidi ya hayo, wananchi wake ni wachapakazi na wanazo stadi za kutosha za ukulima wa kisasa.
- Kwa mujibu wa matokeo ya sensa ya Taifa ya mwaka 2012, idadi ya watu mkoani Simiyu ilikisiwa kuwa 1,591,000. Ukiwa mkoa mpya wenye maeneo yenye uwezekano wa kuwekeza ni wazi kuwa idadi ya watu inaongezeka kila siku na kwa hiyo upanuzi wa huduma za kijamii na uchumi unahitajika.
- Pato la kila mtu katika mkoa huu ni shilingi 510,023/- ukiwa ni miongoni mwa mikoa yenye watu wa kipato cha uchumi wa kati katika nchi. Kilimo kimeendelea kuwa ndiyo shughuli kuu ya kimaisha na kiuchumi ya Mkoa wa Simiyu. Sekta hii inachangia asilimia 75 ya uchumi wa Mkoa huu na inaajiri kiasi cha asilimia 80 ya wananchi katika Mkoa huu. Mazao makuu ya biashara yanayolimwa ni pamba, karanga na alizeti. Mazao makuu ya chakula ni mahindi, mtama, mpunga, viazi vitamu, ulezi na muhogo.
- Usafiri wa kuunganisha mkoa huu na mikoa mingine na ukaribu wake na nchi za jirani ni jambo jingine muhimu linalowavutia wawekezaji katika mkoa huu.
- Wawekezaji wanakaribishwa kuwekeza katika viwanda vya pamba. Mtu anapozungumzia uzalishaji wa pamba nchini Tanzania, mtu huyo atakuwa anazungumzia pamba ya Maswa katika Mkoa wa Simiyu. Kwa mujibu wa takwimu, hadi sasa mkoa wa Simiyu ndiyo Mkoa unaoongoza katika uzalishaji wa pamba nchini Tanzania ukizalisha zaidi ya tani 150,000 za pamba yenye mbegu kwa mwaka. Wawekezaji wanakaribishwa kuwekeza katika kilimo cha pamba na viwanda vya kuchambulia pamba na shughuli nyinginezo.

- Wawekezaji wanakaribishwa vile vile kuwekeza katika viwanda vya mifugo; ufugaji ni shughuli kuu ya pili ya kiuchumi ya mkoa huu. Mkoa wa Simiyu una jumla ya ng'ombe 1.5 milioni, Mbuzi 674,402, Kondoo 254,746, Kuku 1,501,146 na Nguruwe 1, 723.
- Zaidi ya maeneo hayo mawili muhimu ya uwekezaji yaliyoelezwa hapo juu, wawekezaji wanakaribishwa vile vile kuwekeza katika viwanda vya kusindika samaki pamoja na mbogamboga. Wakulima wa mbogamboga wanahitaji sana mbegu, vifaa vya kufungashia na soko la kuaminika. Hii ni fursa nzuri kwa makampuni/wawekezaji wenyeji na wa kimataifa kuanzisha viwanda vitakavyozalisha vifungashio vya mbogamboga na matunda ili kuikuza biashara hiyo katika eneo hilo.

**SEHEMU YA PILI:**

# HALI YA KIJAMII NA KIUCHUMI YA MKOA WA SIMIYU

## 2.1 Eneo, idadi ya watu na hali ya hewa

Mkoa wa Simiyu upo Kaskazini ya Tanzania na Kusini Mashariki ya Ziwa Victoria, Ukiwepo baina ya Latitudo 2$^{0}$1” na 4$^{0}$0” Kusini ya Ikweta na baina ya Longitudo 33$^{0}$3” na 35$^{0}$1” Masharki ya Greenwich. Mkoa huu una eneo la kilomita 23,807.7 za mraba na kiutawala una Wilaya 5, Manispaa 6, Tarafa 16, Kata 109 na Vijiji 471. Kwa mujibu wa sensa ya Taifa ya Idadi ya Watu ya mwaka 2012 idadi ya watu wa Mkoa wa Simiyu ilikuwa 1,584,157 ikiwa ni kiasi cha ongezeko la watu la asilimia 1.8 kwa mwaka.


Mkoa huu unapakana na Mikoa ya Manyara na Singida upande wa Mashariki, Mkoa wa Shinyanga upande wa Kusini, Mkoa wa Mwanza upande wa Magharibi, na Mkoa wa Mara upande wa Kaskazini. Kwenye mpaka wake wa upande wa Mashariki na sehemu ya mpaka wake wa upande wa Kaskazini unapakana na mbuga maarufu za taifa za Serengeti na Ngorongoro. Mkoa wa Simiyu una hali ya hewa ya wastani wa nyuzi joto kati ya 18$^{0}$C hadi 31$^{0}$C kila mwaka. Hata hivyo Mkoa huu una msimu mmoja wa mvua ambao kwa kawaida huanza mwezi Oktoba na kumalizika Mei. Msimu wa mvua hugawika katika misimu midogo miwili. Wa kwanza huanza mwezi Oktoba na kumalizika mwezi Desemba na wa pili huanza Februari hadi katikati ya mwezi Mei, huu ukiwa ndiyo msimu mrefu. Kwa ujumla msimu wa mvua hauna uiano na hautabiriki, kawaida huwa kati ya mm 600 hadi mm 900. Topografia ya Mkoa huu ni ya ardhi tambarare, nyanda za miteremko midogo na uoto mdogomdogo wa hapa na pale na sehemu fulani zina mapori ya miti ya Miombo. Udongo wa mkoa huu ni mzito na mweusi (*mbuga*) na maeneo fulani yana udongo mwekundu na mengine udongo wa kichanga.

## 2.1 Kanda za ekolojia ya kilimo

Mkoa wa Simiyu una kanda tatu za ekolojia ya kilimo. Kanda ya kwanza

inajumuisha Wilaya za Bariadi, Busega na Itilima, zenye topografia ya kupanda na kushuka zenye udongo mfinyanzi na udongo wa juu mweupe. Kiasi cha mvua ni baina ya mm 700 - 900. Shughuli kuu ya kiuchumi katika kanda hii ni pamoja na kilimo cha mazao hasa mahindi, mtama, pamba, muhogo na ufugaji. Kanda ya pili inajumuisha Wilaya ya Meatu yenye topografia ya kupanda na kushuka na kupindapinda upande wa Mashariki wenye udongo mfinyanzi wenye rutuba. Kanda hii ina mmomonyoko mbaya wa udongo unaopunguza kilimo cha mazao. Kiasi cha mvua kwa kawaida ni chini ya mm 700 chenye tabia isiyotabirika. Kilimo cha mazao na ufugaji ndiyo shughuli kuu za kiuchumi katika eneo hili. Mazao makuu yanayolimwa katika eneo hili ni pamoja na mtama, pamba na mahindi. Kanda ya tatu inajumuisha Wilaya ya Maswa yenye topografia ya kupanda na kushuka na ya kupindapinda. Ardhi yake ni ya udongo wa Usukumani maarufru kwa jina la *mbuga,* udongo mfinyanzi mweusi wa tifutifu ambao ni mzuri kwa kilimo cha mpunga. Mazao mengine yanayolimwa katika eneo hili ni pamoja na mahindi, mtama na pamba. Kanda hii ina kiasi cha mvua kisichoaminika kati mm 700 hadi mm 800 kwa mwaka. Eneo hili ni maarufu pia kwa shughuli za ufugaji.

**Kielelezo 1.1: Ramani ya Mkoa wa Simiyu**



**SEHEMU YA TATU:**

# FURSA ZA UWEKEZAJI ZA KIPAUMBELE MKOANI SIMIYU

Hapa chini ni muhtasari wa aina kuu mbili za fursa za uwekezaji, ambazo ni fursa kuu za uwekezaji wa kimkakati[1] na fursa mahasusi za uwekezaji.

## 3.1 Fursa kuu za uwekezaji wa kimkakati katika Mkoa wa Simiyu

Simiyu ni miongoni mwa mikoa ya Tanzania yenye fursa za kuvutia za uwekezaji, kilimo kilichochangamka na uzalishaji wa mifugo, pamoja na mandhari za kuvutia watalii katika hifadhi ya wanyama ya Maswa ambayo ni sehemu ya eneo la hifadhi ya Ngorongoro na mbuga ya wanyama ya Taifa ya Serengeti. Sehemu ya Ziwa Viktoria katika Mkoa huu inawezesha kufikiwa kwa urahisi soko la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwa kupitia bandari kuu nne.; unapakana na Kenya ambayo ndiyo soko kubwa kuliko yote kwa bidhaa mbalimbali katika Afrika ya Mashariki.

Mkoa huu unazalisha nusu ya uzalishaji wote wa Tanzania wa pamba yenye mbegu na una ng'ombe zaidi ya milioni 1.5, mbuzi 700,000 na kondoo 300,000. Zaidi ya hayo, Simiyu yenye hekta milioni 24 za ardhi yenye rutuba ni miongoni mwa wazalishaji wakuu watano wa mpunga, choroko, mahindi, alizeti, nyama, maziwa na ngozi.

Mkoa huu umepanga kuchochea maendeleo yake ya viwanda na kuimarisha msingi wake wa kiuchumi kwa kuvutia uwekezaji wa ziada wa ubia kwa watu binafsi na serikali ili kuimarisha uwezo wake wa kutengeneza bidhaa za viwandani na uwezo wake wa kuhimili ushindani na kuinua

[1] Uwekezaji ambao utakuwa na tija baada ya muda by a that is intended to make it more over , for in a new that new or that is new; uwekezaji ambao shirika au kampuni zilizojiunga nazo wanaunda kampuni mpya changa yenye nia ya kujenga kitu kitakachokuwa na thamani kwa shirika lenyewe; kadhalika uwekezaji wa kimkakati ni muamala ambao unakaribiana na ubia au ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Kwa uwekezaji wa kimkakati, kampuni moja inawekeza katika kampuni nyingine. Kampuni mbili hizi zinaingia katika makubaliano yenye nia ya kutekeleza malengo ya kibiashara ya pamoja

uzalishaji wake wa ndani wa Jumla. Serikali ya Mkoa na mamlaka za Wilaya ziko tayari na zimejitolea kutoa huduma mbalimbali za ziada za msaada na motisha kwa wawekezaji ili kusukuma maendeleo ya viwanda na ukuwaji wa uchumi kwa vipindi vya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu.

Fursa kuu za uwekezaji wa kimkakati katika Mkoa wa Simiyu kwa vipaumbele ni:

1. Ujenzi wa malambo ya kina kifupi, malambo ya juujuu, ujenzi wa mfumo wa kuvuna maji ya mvua na uchimbaji wa visima virefu vyenye uwezo wa kusambaza mita za ujazo milioni 150-160 za maji kwa kila wilaya kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na matumizi ya viwandani (Angalizo: ijapokuwa bomba la maji la kutoka Ziwa Victoria kwa kupitia kwenye matanki ya maji yaliyojengwa juu ya Kilima cha Ngasamo hadi wilayani limedhamiriwa kuwa kwa jili ya usambazaji wa maji majumbani lakini usambazaji utakuwa ni km 12 tu kutoka kwenye bomba kuu na asilimia 40 - 50% ya vijiji ndiyo watakaoweza kuyafikia maji hayo).
2. Mabwawa ya kuhifadhi maji na Mipango ya Kilimo cha Kumwagilia chenye kunusuru maji kwa ajili ya uzalishaji wa mpunga, mazao ya mbogamboga, mahindi na pamba katika wilaya za Busega na Bariadi**.** Kuongeza uzalisha wa kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia mitambo na kuhakikisha uzingatiaji wa hali ya hewa.
3. Kuanzisha mashamba ya kilimo cha kibiashara ya mtu mmoja mmoja au vikundi kwa ajili ya uzalishaji wa pamba yenye ubora wa hali ya juu yatakayoweza kuzalisha tani 700,000 - 800,000 za pamba yenye mbegu kwa ajili ya uzalishaji wa ndani wa vitambaa, bidhaa za afya ya viumbe hai na usafi, bidhaa za matumizi ya shule, vifaa kwa ajili ya biashara ya kukaribisha wageni, na kwa kusafirisha nchi za nje ifikapo mwaka 2040.
4. Viwanda viwili vya kisasa vya kuchambulia pamba kimoja Meatu na kingine Maswa, na kiwanda cha kutengeneza vitambaa Meatu na/au Maswa.
5. Viwanda vya kusaga/kukoboa na kufungasha mchele, mahindi, dengu, choroko na mbaazi; Lamadi, Bariadi, na Maswa.

6. Vituo vya mafunzo kwa ajili ya kuzalisha rasilimali watu wenye stadi za ngazi ya kati na ngazi ya juu:
   a. Vituo vya mafunzo ya kilimo na ufugaji Meatu na Maswa;
   b. Ujenzi wa majengo ya shule kwa ajili ya masomo ya sayansi kwa shule za sekondari katika wilaya zote;
   c. Kuwekeza katika Asasi za Mafunzo ya Tiba Itilima,
   d. Vyuo vya Walimu Zanzui, Itilima;
   e. Matawi ya Taasisi za Elimu ya Ufundi na Vyuo Vikuu vya Uhandisi kwa wenye vipaji maalum Bariadi, Maswa, na Meatu.

7. Viwanda vya kuzalisha mafuta ya kupikia ya mbogamboga na vya kusafisha mafuta ya alizeti kwa matumizi ya binadamu na mafuta ya mbegu za pamba kwa uzalishaji wa diseli huko Meatu, Bariadi, na Busega.
8. Huduma za matibabu ya mifugo huko Meatu, Maswa, Itilima, na Bariadi.
9. Kuanzishwa kwa kiwanda cha nyama  Wilaya ya Meatu, Mashamba ya Kulisha Mifugo, Ranchi ndogo kwa ajili ya kunenepeshea, masoko madogo ya kisasa kwa ajili ya mifugo, kiwanda cha Nyama ya kuku na Mayai Meatu, Maswa, na Miji ya Bariadi.
10. Viwanda vya ngozi huko Meatu, Maswa na Bariadi.
11. Viwanda kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa za ngozi Meatu, Maswa, Itilima, na Bariadi.
12. Uzalishaji wa kuku wa kienyeji kwa ajili ya mayai na nyama na kuku wa kisasa Maswa, Bariadi, Busega, na Itilima.
13. Viwanda vya bidhaa za maziwa Maswa na Meatu (unafanywa utafiti wa upanuzi wa Meatu Milk).
14. Ugavi wa umeme wa MW 400-500 kutoka gridi ya taifa, uzalishaji wa umeme kutokana na makaa ya mawe, gesi asilia na paneli za kuzalisha umeme wa mwanga wa jua huko Meatu, Itilima, Maswa na Busega ifikapo mwaka 2050.
15. Maeneo ya viwanda matatu yaliyounganishwa kati ya Lamadi na Bariadi (50km x 60km), kati ya Maswa na Malampaka, 30 km x30 km; kati ya Mwandoya na Ngoboko, 30km x 30km Meatu; kati ya

Lagangabilili na Lugulu, 15km x 15km Itilima; na eneo la kutengeneza bidhaa za kusafirisha nje hapo Malampaka (Halmashauri ya Wilaya ya Maswa).

16. Ujenzi wa nyumba zenye ubora na za bei nafuu katika makao makuu ya wilaya zote, maduka makubwa, kumbi za mikutano na ofisi kwa ajili ya kukodisha.
17. Utalii: Kuanzisha maeneo ya wanyama pori, ranchi za wanyama pori, vitalu vya mawindo, maeneo ya kupiga kambi na hoteli katika Hifadhi ya Wanyama Pori ya Maswa, kwa ajili ya kuona wanyama, kupiga picha, matembezi, utalii wa kimazingira na utalii wa kiutamaduni katika wilaya za Meatu na Maswa.
18. Ujenzi wa gati na kituo cha burudani cha Nyamikoma, usafiri wa majini, kuangalia ndege wanaoishi kwenye maji, kupiga mbizi ndani ya maji ya kina kirefu, michezo ya kuvua samaki na ujenzi wa kituo cha michezo ya ndani ya maji wilaya ya Busega.
19. Ufugaji wa samaki kwa kutumia vizimba na matanki *(RAS)* katika wilaya za Busega na Bariadi kukidhi mahitaji yanayotokana na ongezeko la idadi ya watu; kupunguza uharibifu wa mazingira ya Ziwa Victoria kutokana na uvuvi haramu, kuongeza uzalishaji wa samaki kwa ajili ya masoko ya ndani na nje;
20. Ujenzi wa masoko ya kisasa, yenye huduma za minada ili kujenga mazingira mazuri na nafasi ya kutosha kwa ajili ya biashara; huduma za kifedha na za kibiashara; maeneo makubwa ya karakana na maegesho ya magari na; (~200 malori), maghala ikiwa ni pamoja maghala yenye ubaridi;
21. Upandaji miti kwenye wilaya zote, miti ya asili na ya kisasa inayokua kwaharaka.
22. Hoteli (nyota 2-3) huko Bariadi, Maswa, Lamadi na Meatu, na hoteli za nyota 4 kwenye hifadhi za wanyama pori ya Maswa na Lamadi - Busega. (karibu na Serengeti).
23. Hospitali na Kliniki za utaalamu maalum katika kila Wilaya.
24. Ujenzi na uboreshaji wa maeneo ya michezo pamoja na huduma za michezo (viwanja vya kuchezea, vyuo vya michezo, maduka ya vifaa vya michezo) ili kuendeleza michezo na ustawi wa watu wa Simiyu.

25. Maeneo ya kushughulikia taka ngumu na ukusanyaji wa taka ngumu na za majimaji na jinsi ya kuzishughulikia.
Kuanzisha viwanda vya kusindika nyanya na mazao mengine ya mbogamboga huko Lamadi katika Halmashauri ya Wilaya ya Busega, kuongeza thamani mazao, kupunguza hasara za uharibifu baada ya mavuno kwa wenyeji.

## 3.2 Fursa mahsusi za uwekezaji mkoani Simiyu

### *1. Mifumo ya ugavi wa maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, ufugaji wa samaki, viwanda, mifugo na matumizi ya nyumbani*

| Muhtasari wa Fursa | |
|---|---|
| **Mambo muhimu** | • Ujenzi wa malambo ya kina kifupi, malambo ya juujuu, ujenzi wa mfumo wa kuvuna maji ya mvua na uchimbaji wa visima virefu vyenye uwezo wa kusambaza mita za mjazo milioni 150 - 160 za maji kwa kila wilaya kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, mifugo, matumizi ya nyumbani na matumizi ya viwandani<br>• Kuwekeza katika uvunaji wa maji ya mvua, uhifadhi wa maji na urejeleaji na teknolojia za kutibu maji taka. |
| **Mantiki ya uwekezaji huu** | • Uhaba wa maji unaoathiri uzalishaji na utoaji wa mazao na uzalishaji wa mifugo;<br>• Kukosekana maji vijijini huathiri afya na usafi wa mazingira<br>• Maendeleo ya viwanda yatakuwa ya shida kwa ajili ya upungufu wa maji.<br>• Mabadiliko ya kiasi cha mvua huathiri msukumo wa maji chini ya ardhi. |
| **Msaada uliopo** | • Msaada mkubwa kutoka Wizara ya Maji na Umwagiliaji na mamlaka za wilaya;<br>• Msaada kutoka kwa Wadau wa maendeleo na Vyombo Visivyo vya Kiserikali (NSAs)<br>• Shauku inayozidi kukua ya serikali; Vipaumbele vya Sera ya Taifa kama vile Dira ya Taifa 2025 na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano |
| **Changamoto/ Vihatarishi na hatua za kukabiliana nazo** | • Uwekezaji wenye kujali mtaji;<br>• Kasma ndogo kutoka serikalini kwa ajili ya maji;<br>• Viwango vya changamoto<br>• Ukosefu wa ujuzi juu ya namna ya kuhifadhi maji na teknolojia ya namna ya kuyarejelea, na mbinu za kuyatumia tena maji. |

### *2. Mabwawa ya kuhifadhi maji na Mipango ya Kilimo cha Kumwagilia chenye kunusuru maji*

| Muhtasari wa Fursa | |
|---|---|
| **Mambo muhimu** | Ujenzi wa mabwawa ya kuhifadhi maji na mipango ya kilimo cha umwagiliaji na njia za umwagiliaji wa kiasili (kiasi cha Ha. 30,000 - 40,000) kwenye Wilaya za Busega, Bariadi, |

| | |
|---|---|
| | Itilima na Maswa, kwa kilimo kwenye mashamba ya wazi na shamba kitalu kwa ajili ya uzalishaji wa mazao yanayohitajika sana na yenye thamani kubwa, chakula cha mifugo na ufugaji wa samaki ifikapo mwaka 2035,<br>• Kuanzisha shuguli za kibiashara za kisasa za mbogamboga, matunda, viungo na mbegu za kilimo cha bustani kwa masoko ya hapa nchini, ya kanda na ya kimataifa;<br>• Kuazisha vikundi kwa ajili ya miradi ya uzalishaji wa mpunga vitakavyolima kiasi cha hekta 10,000 au zaidi kwa uzalishaji wa tani > 10 tons kwa hekta (uzalishaji wa sasa wa mpunga kimkoa kwa mwaka ni tani > 400,000);<br>• Kuanzisha biashara za kukoboa mpunga, kufungasha na kutafuta masoko;<br>• Kuanzisha ufugaji wa samaki kwenye mabwawa yaliyojengwa;<br>• Kuanzisha uzalishaji wa chakula cha mifugo kwa kutumia njia ya kuotesha mimea kwenye maji.<br><br>Uzalishaji unaotarajiwa/matokeo:<br>• Mpunga, mbogamboga, chakula kwa ajili ya ng'ombe na wanyama wadogo wanaocheua, samaki kwa matumizi ya ndani, biashara, na bidhaa za kusafirisha nje katika nchi za jirani za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, COMESA na SADC na nchi za nje;<br>• Maji kwa ajili ya mifugo;<br>• Udongo ulioboreshwa na usimamizi wa maji;<br>• Mchango katika upatikanaji endelevu na usalama wa chakula na lishe kimkoa na kitaifa;<br>• Uongezaji wa juhudi za kupunguza umasikini kwa upatikanaji wa fursa za ajira zenye tija na uzalishaji wa kipato endelevu wakati wa utekelezaji / ujenzi wa mabwawa, mipango, miundo na shughuli za uzalishaji. |
| **Mantiki ya uwekezaji huu** | • Msaada mkubwa wa kisiasa kimkoa na kitaifa – unaoongozwa na Seketariet ya Mkoa, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Wizara ya Kazi, Usafirishajl na Mawasiliano, TAMISEMI, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu na wadau wa Maendeleo;<br>• Maji yenye ubora kwa wingi kutoka Ziwa Victoria, kiasi cha mvua (mm 600-800 kwa mwaka);<br>• Kuna mahitaji makubwa kwa mazao ya bustani yenye ubora kwa soko la hapa ndani na soko la nje; huko; Meatu, Mbuga ya Taifa ya Wanyamapori ya Serengeti, eneo la hifadhi la Ngorongoro,<br>Shinyanga, Mwanza, na Kenya;<br>• Mkoani simuyu bado kuna upungufu mkubwa wa bidhaa zenye ubora na hivyo kuufanya Mkoa huu uagize kutoka nje matunda, mbogamboga na viungo kama vile nyanya, vitunguu, vitunguu swaumu, n.k;<br>• Uwezekani wa kufaidika kwa pande zote husika (Ubia kati ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma "PPP");<br>• Hali ya kubadilikabadilika ya kiasi cha mvua, ukame wa mara kwa mara na usimamizi wa udongo na maji hizi zikiwa ni changamoto zinazotishia usalama wa chakula na lishe, biashara na ustawi wa wananchi mkoani Simiyu; |

| | |
|---|---|
| | • Utayari wa Serikali kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi, mpango kabambe wa umwagiliaji, utaratibu wa haki ya matumizi ya maji, kushughulikia vikwazo vinavyoweza kujitokeza, n.k;<br>• Upatikanaji wa masoko: mkoani, nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, COMESA, na SADC;<br>• Motisha za kuvutia, kama zinavyotolewa na Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania, Mwongozo wa Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania 2014; |
| **Msaada unaoweza kupatikana** | • Msaada unaoweza kupatikana wa kiufundi, kujenga uwezo, mambo yanayohusu uingizaji na utoaji na msaada mwengine wa rasilimali kutoka katika Mipango ya Maendeleo ya Wilaya na Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo II (ASDP 2017-2021), na kasma za bajeti za kisekta;<br>• Mafunzo, teknolojia, biashara, mambo yanayohusu uingizaji na utoaji, na taasisi za fedha zinazosaidia maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji kama vile Benki ya Dunia, AfDB, EADB, Kilimo Trust, EU, JICA, KOICA, SNV, BMGF, CSO, vyama visivyokuwa vya Kiserikali vya hapa nchini na vya nchi za nje, n.k;<br>• Shauku ya umma inayozidi kukua; vipaumbele vya Sera ya Taifa kama vile Dira ya Taifa 2025 na Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Miaka Mitano |
| **Changamoto/ Vihatarishi na hatua za kukabiliana nazo** | • Mkataba wa Maji ya Mto Nile wa 1929 ambao unaizuia Tanzania kuyatumia maji ya Mto Nile kwa madhumuni ya kilimo cha umwagiliaji inabidi ufanyiwe marekebisho;<br>• Uwezekano wa kuwepo kwa changamoto za utunzaji za muda mrefu miongoni mwa watumiaji wa mwisho;<br>• Zinahitajika juhudi kubwa za kujenga uwezo;<br>• Uelewa mkubwa na miradi yenye kujali mitaji na shughuli zake;<br>• Msaada wa kiufundi na kifedha kutoka nje, mafunzo na utendaji ulio bora kabisa kutoka kwa wale walio bora kabisa darasani na maarifa ya asili yaliyoboreshwa yanahitaji yatumiwe |

## *3. Uzalishaji wa pamba yenye ubora wa hali ya juu*

| Muhtasari wa Fursa | |
|---|---|
| **Mambo Muhimu** | Uzalishaji endelevu wa pamba yenye ubora wa hali ya juu Meatu na wilaya nyingine kulingana na viwango na mahitaji ya watumiaji/wanunuzi, Taratibu za Udhibiti za Bodi ya Pamba ya Tanzania, viwango vya ubora wa mazao kwenye shamba la wazi la hekta 50,000 - 80,000 lenye mazingira ya kumwagiliwa.<br>1. Uwekezaji kwenye mashamba makubwa na ya wastani ya kuzalisha pamba huko Maswa na Meatu, ambako wakulima tayari wamekuwa wakiendesha kilimo cha kutumia samadi na wana ujuzi kamili wa kuendesha kilimo cha kutumia samadi.<br>2. Uwekezaji katika mashamba ya pamba madogo na ya wastani huko Bariadi na Itilima, maeneo yenye udongo mwingi mweusi ambao ni mzuri kwa kilimo cha pamba lakini yanazalisha > katika ekari / 1,000, na uzi wa pamba wenye urefu wa > mm 28.7; |

| | |
|---|---|
| | Uzalishaji unaotarajiwa/matokeo:<br>• Uwekezaji pale kwenye upatikanaji endelevu wa nyenzo za kutosha zenye ubora na kwa wakati ili kuongeza uzalishaji kwa kiwango kikubwa wa mahitaji makubwa ya nyuzi za pamba na mazao ya pamba yaliyoengezewa thamani na mazao mengine ya ziada yanayotokana na pamba;<br>• Uzalishaji wa malighafi za viwandani kutokana na mazao ya ziada yanayotokana na pamba.<br>• Lengo ni Mkoa wa Simiyu uzalishe tani 700,000 - 800,000 za mbegu za pamba ya kawaida na iliyotumia samadi ifikapo mwaka 2040 kwa ajili ya uzalishaji wa vitambaa na nguo, vifaa vya sekta ya afya, vifaa vya usafi, vifaa vya shule, vifaa vya hospitali na kwa kusafirisha nchi za nje. |
| **Mantiki ya uwekezaji huu** | • Simiyu ndiyo Mkoa unaozalisha pamba nyingi kuliko mikoa yote inayozalisha pamba na unachangia asilimia 47% ya pamba yote nchini;<br>• Upatikanaji wa miti ya asili inayofaa kwa kutengenezea dawa za kuulia wadudu kama vile Mwarobaini, Lantana Camara, Mrenaha, Solanium, matumizi ya Mboji ambazo humpunguzia mkulima gharama za uzalishaji;<br>• Hali nzuri ya hewa kwa wastani nyuzi joto 20-30 $^{o}$C, na kiwango cha mvua cha mm 600-900 kwa mwaka (ijapokuwa hubadilikabadilika);<br>• Unatoa mchango katika kufufua na kuendeleza viwanda vya nguo kimkoa na kitaifa;<br>• Unatoa mchango katika juhudi za kuondoa umasikini kwa kuboresha uwezo wa kulipa thamani zao la pamba na kuzalisha ajira zenye heshima na fursa za kuzalisha kipato;<br>• Bidhaa zitokanazo na pamba zinaingiza fedha nyingi za kigeni;<br>• Uzalishaji wa sasa unabadilikabadilika na hautoshi kulipia gharama za uzalishaji;<br>• Uzembe katika uzalishaji, matumizi madogo ya pembejeo, uendeshaji mashamba bila ya kujali gharama na mavuno kidogo ya k.g 300 kwa eka (kiwango cha juu kabisa k.g 700-800 kwa eka), kwa shamba la kawaida eka $< 20$, linaweza sana kuboresha uzalishaji wake (uzalishaji wa kimataifa ni k.g $>$1,500 kwa eka);<br>• Vikundi vya Wakulima Wafanyabiashara (FBGs) vimeanza kuibuka na wamiliki wa viwanda vya kusafisha pamba tayari wapo;<br>• Thamani kubwa na faida ya kuendelea vinaweza kupatikana kwa kuwekeza katika ugavi wa teknolojia inayofaa na inayolipa, mitambo, teknolojia ya kusindika na kufungasha na vifaa vyake, huduma za msaada wa kibiashara na kitaalam, maghala ya kuhifadhia bidhaa, usafirishaji na bidhaa za ziada zilizoongezewa thamani;<br>• Uwezekano wa kuwekeza katika uzalishaji wa mbegu;<br>• Uwezekano wa kuchangia katika kuandaa na kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Viwanda vya Nguo na Vitambaa, Mkakati Uliounganishwa wa Kuendeleza Viwanda 2025, Sera ya Taifa ya Kilimo 2013, na FYDP II;<br>• Uwezekano wa Kufaidika kwa pande zote husika katika mpango wa Ushirikiano kati ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umaa PPP, na Dhima ya Kijamii kwa Shirika Linalowekeza (CSR);<br>• Upatikanaji wa soko katika nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, SADC, na nchi za nje; |

| | |
|---|---|
| | • Imani na kuwepo kwa uhusiano mkubwa wa kiutamaduni katika shughuli za uzalishaji pamba kati ya wazalishaji wadogo. |
| **Msaada uliopo** | • Msaada mkubwa wa kisiasa kutoka kwa Rais na viongozi wa mkoa na wilaya, Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, vyama vya sekta binafsi na wadau wa maendeleo kama vile Gatsby Charity Foundation, DfID, COMPACI, RLDC, Cotton made in Africa,TIC na Vyama Visivyokuwa vya Kiserikali (NGOs); shauku ya wananchi inayozidi kukua; Vipaumbele vya Sera ya Taifa kama vile Dira ya Taifa 2025 na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano"Kutoka Pamba hadi Kitambaa";<br>• Msaada endelevu wa kifedha lakini mdogo kutoka serikalini, mamlaka za wilaya na ASDP II;<br>• Msaada thabiti wa R&D kutoka katika Taasisi ya Utafiti ya Ukiriguru ya Mwanza, yenye uzoefu wa muda mrefu katika utafiti wa pamba na usambazaji wa huduma bora za ufundi;<br>• Upataji bora wa huduma za fedha za kimataifa kwa ajili ya uwekezaji kama nyongeza ya sera, kitaasisi, biashara, uzalishaji, thamani, na uboreshaji wa mazingira ya kibiashara;<br>• Ushindani mkubwa kutoka katika misisimko ambayo ina bajeti ndogo za mashamba na bei bora zaidi mara 2 - 3;<br>• Mikopo mizuri kutoka katika Benki ya Kilimo Tanzania, AfDB, n.k. |
| **Changamoto/ Vihatarishi na hatua za kukabiliana nazo** | • Tofauti kubwa ya bei ya msimu ( ukomo wa Sh. 800 - 1200 kwa kg kulingana na Bodi ya Pamba Tanzania) na anguko la bei duniani kuwafanya wazalishaji kutoa mbegu za pamba zenye ubora mdogo;<br>• Kupungua kwa mbolea katika ardhi, kujaa kwa viumbe waharibifu;<br>• Athari za tabia nchi zinaweza kuathiri zaidi uzalishaji katika mifumo ya uzalishaji ya mvua;<br>• Kiufundi na kifedha taasisi zenye msaada dhaifu (mf., Mfuko wa Maendeleo ya Pamba Tanzania (CDTF), Chama cha Pamba Tanzania) ambazo zinahitaji kuimarishwa;<br>• Mzunguko dhaifu wa usambazaji wa pembejeo; kujenga uwezo imara katika uwezo wa ufundi wa pamba na uongozi wa shamba wa watu binafsi na makundi ya wakulima kunahitajika;<br>• Changamoto za usafirishaji, nishati, maji, na rasilimaliwatu waliofundishwa/wenye ujuzi katika baadhi ya maeneo;<br>• Haja kubwa ya kurekebisha mkataba[1] unaohusu mfumo wa ukulima, usambazaji wa pembejeo za mashambani, miundombinu ya masoko, kuelezea masuala makubwa na |

2 Wakati ukulima wa mikataba hasa katika pamba unaonekana kuwa na changamoto, ipo fursa ya uwekezaji hasa kwa wawekezaji katika vinu vya kuchambulia pamba na viwanda vya nguo; fursa hii itaboreka sasa ambapo serikali inarekebisha mfumo wa udhibiti wa mikataba ya ukulima ambayo italeta faida kwa wadau wote wa mzunguko wa thamani ya nguo; kutakuwa na fursa pia kwa mikataba katika kilimo cha bustani, alizeti kwa ajili ya mafuta ya kula, na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa katika sehemu nyingi za Tanzania ikiwa ni pamoja na Simiyu.

| | |
|---|---|
| | kushuka na kupanda kwa bei ya sokoni ya pamba, na kuboresha teknolojia ya kinu cha kuchambulia pamba, kuimarisha ufanisi katika mzunguko wa thamani wa pamba ya Simiyu;<br>• Uingiliaji muhimu wa Serikali ya Tanzania na sekta binafsi unahitajika kushughulikia vikwazo na vihatarishi vya hapo juu; na<br>• Mfumo dhaifu wa udhibiti. |



*Shamba la Pamba*

## Jedwali la 3.1: Utabiri wa uzalishaji wa mazao makuu katika msimu wa 2016/2017 katika Mkoa wa Simiyu

| Zao | Utabiri wa wingi wa mazao kwa Wilaya katika mwaka 2016/2017, MT | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Meatu | Maswa | Itilima | Busega | Bariadi | Bariadi TC* |
| **Mahindi** | 73,288 | 98,816 | 87,860 | 43,189 | 99,420 | 20,858 |
| **Mpunga** | 12,368 | 41,851 | 21,009 | 25,929 | 32,912 | 14,197 |
| **Mtama** | 77,252 | 69,752 | 24,490 | 16,504 | 8,773 | 2,592 |
| **Viazi vitamu** | 48,857 | 29,064 | 27,307 | 21,434 | 43,927 | 6,995 |
| **Choroko** | 5,135 | 13,950 | 2,463 | 1,657 | 13,774 | 508 |
| **Dengu** | 1,932 | 17,438 | 7,004 | 948 | 14,764 | 230 |
| **Mbaazi** | 1,196 | 7,440 | 3,985 | 10 | 1,343 | 1,838 |
| **Pamba** | 51,321 | 81,378 | 45,787 | 35,065 | 65,296 | 40,072 |

*Halmashauri ya Mji wa Bariadi

*Chanzo: Ofisi ya Mkoa wa Simiyu, 2016*

*Uwezo wa uzalishaji wa chakula na mazao ya biashara katika Mkoa wa Simiyu upo chini ukilinganisha na viwango vya dunia. Matumizi ya mbegu bora, zenye kutoa mazao mengi na zinazomudu mazingira na tabia nchi, mbolea bora, teknolojia, utumiaji wa mitambo, umwagiliaji, usimamizi bora wa baada ya mavuno, na uhifadhi katika maghala inaweza kuongeza uzalishaji mara dufu katika miaka mitatu au minne ya mzunguko wa uzalishaji.*

## 4. Vinu vya kisasa vya uchambuaji wa pamba na vinu vya nguo: Uzalishaji wa pamba –unaolenga katika nguo na mavazi na bidhaa kwa ajili ya sekta ya elimu, na viwanda vya afya na ukarimu

| Maelezo ya fursa | |
|---|---|
| **Mambo Muhimu** | • Uanzishaji wa vinu vya kisasa vya kuchambulia pamba vyenye mchakato wa ufanisi wa teknolojia, angalau kimoja katika kila wilaya;<br>• Uwekezaji katika Viwanda vya nguo/mavazi kuzalisha nguo na mavazi ya pamba na bidhaa kwa ajili ya sekta ya elimu, na tasnia ya afya na ukarimu;<br>• Uanzishaji wa mitambo ya kusokotea nyuzi na ufumaji. |
| **Mantiki ya uwekezaji huu** | • Simiyu inazalisha zaidi ya 47% ya mbegu za pamba nchini Tanzania, kuhakikisha usambazaji wa kawaida na wa ufanisi wa nyuzi za pamba katika vinu vya kuchambulia pamba na malighafi, mf. nyuzi zilizosokotwa na vitambaa katika viwanda muhimu katika mzunguko wa thamani ya nguo na mavazi;<br>• Kwa sasa, vinu vya kuchambulia pamba vinafanya kazi kwa miezi 2 - 3 kwa sababu ya uhaba wa mbegu za pamba;<br>• Daraja la watu wenye kipato cha kati linaloibuka linasukuma mahitaji ya nguo bora;<br>• Tasnia ya nguo Tanzania kwa sasa ina ukomo sana katika ukubwa na bidhaa zinazotolewa;<br>• Haja ya soko: Kuna haja kubwa kwa ajili ya kufuma vitambaa ndani ya soko la ndani kuondoa kiasi kikubwa kinachoingizwa kutoka nje - pia kuna umuhimu katika masoko ya kimkoa, mf. kwa zuio linalokuja la kuingiza mitumba (nguo zilizotumika) katika Jumuiya ya Afrika Mashariki;<br>• Tanzania ina historia ndefu katika uzalishaji wa nguo na mavazi inarudi nyuma mpaka miaka ya mbali ya 1966 na kutoa fursa kwa ongezeko la thamani kutoka ugani mpaka viwandani.<br>• Simiyu ina sera nzuri na mazingira ya kibiashara kuwa eneo kubwa la uwekezaji wa nguo na mavazi;<br>• Eneo bora kwa ajili ya kuwekeza katika biashara, mchakato wa kiteknolojia, na mifumo ya uzalishaji;<br>• Kuna soko muhimu linalofaa kwa nguo na mavazi ya Tanzania katika masoko ya ndani, kimkoa na kimataifa, ikiwa ni pamoja na faida ya kufikia katika soko la Marekani kupitia Sheria ya Ukuaji wa Kiafrika na Fursa - AGOA;<br>• Nguo nyingi zinazonunuliwa nchini Tanzania zinaingizwa nchini kutoka nje. Kwa sasa kuna mauzo ya vitenge na kanga tu na soko dogo la ndani na la mkoa kwa nguo za Tanzania, ambalo lina ukomo katika uhamasishaji wa nguo na kofia; |

| | |
|---|---|
| | • Nafasi kubwa za upenyaji wa soko katika vifaa vya kiafya kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati kwani nchi zote hizi zinaingiza vifaa hivyo vya kiafya. Hakuna hata moja ya nchi hizi ambayo imewekeza katika vifaa vya kiafya vya viwanda vya nguo;<br>• Pamba nyingi ya Tanzania inayosafirishwa nje inajumuisha zaidi vitambaa vya pamba (87%), ikifuatiwa na nyuzi za pamba (8%) na ufumaji wa vitambaa (5 %). Upelekaji nje wa vitambaa vya pamba ni sawa na 62% ya jumla ya nguo za Tanzania na upelekaji wa nguo nje, kuonyesha kwamba nyongeza nyingi ya thamani katika pamba ya Tanzania inatokea ughaibuni[2]. |
| **Msaada uliopo** | • Msaada thabiti wa kisiasa kwa mamlaka za kimkoa na wilaya, Wizara ya Viwanda, Biashara, na Uwekezaji (MITI), jumuiya ya biashara, na washirika wa maendeleo kama vile Mfuko wa Hisani wa Gatsby, DFID; shauku inayokua ya umma; vipaumbele vya Sera ya Taifa kama vile Dira ya Taifa ya 2025 na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano<br>• Msaada wa kiufundi na ushauri wa uwekezaji vipo katika Kitengo cha kusaidia tasnia ya Nguo na Mavazi (TDU) huko MITI;<br>• Upataji mkubwa wa fedha za kimataifa kwa ajili ya kuanzisha uwekezaji;<br>• Bei ya ushindani ya nguvukazi (ca. Dola za Kimarekani 1-2/saa), ambayo ni chini ya wastani wa utengenezaji mwingi wa nguo katika Afrika Chini ya Sahara;<br>• Mikopo inayofaa kutoka katika Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB), Benki ya Dunia, AfDB, n.k.;<br>• Wawekezaji wanasaidiwa na motisha kupitia katika punguzo la kodi, kutolipa ushuru wa kuingiza mali za mtaji. |
| **Changamoto/ Vihatarishi na hatua za kukabiliana nazo** | • Wakati mwingine changamoto za madaraja na utokeaji wa ubora dhaifu wa nyuzi za pamba, pamoja na urefu wa nyuzi za pamba katika robota la pamba (wastani wa mm 28), unasababisha matatizo ya ubora kwa uzalishaji mzuri wa nyuzi, na matokeo yake ni ubora dhaifu wa nyuzi kwa viwango vilivyozidi vya uchafu;<br>• Usambazaji unaofaa wa umeme; Gharama kubwa za umeme, mf. nyuzi zinalipa Sh. Milioni 25 - 30 kwa ajili ya umeme katika msimu wa uzalishaji mkubwa;<br>• Ufanisi mdogo na wakati mwingine kushindwa kwa soko la pamba katika michakato ya mzunguko wa thamani;<br>• Kutotosha kwa watu wenye vipaji vya kati kuelekea vya juu vya kiufundi na kibiashara;<br>• Usafirishaji, nishati (usimamishaji wa nishati) miundombinu ya TEHAMA, na changamoto za maji, ambazo zinaweza kusababisha athari kubwa katika ushindani;<br>• Kwa sababu ya kuwa na mahitaji mengi na bei kubwa ya pembejeo, wazalishaji wadogowadogo wa pamba wanalazimika kuhamia katika kilimo cha dengu, choroko, mbaazi, na alizeti na hivyo kuathiri zao la pamba (bei ya pamba ni kati ya |

[3] Katika mwaka 2010, upelekaji nje wa nguo na mavazi ya Tanzania ulifikia thamani ya jumla ya Dola za Kimarekani Milioni 140,7. Nguo za pamba (kitambaa na nyuzi) zilizalisha Dola za Kimarekani Milioni 100,4 (71%) ikifuatiwa na nguo za vitambaa za mimea (HS cat. 53) kwa Dola za Kimarekani Milioni 12,7 (9%) na kitani, kamba, kebo, nyavu (Dola za Kimarekani Milioni 9, 6%). Upelekaji nje wa jumla ulifikia Dola za Kimarekani Milioni 11,6 ambapo Dola za Kimarekani Milioni 8.7 zilitokana na ufumaji na Dola za Kimarekani Milioni 2,9 zilijumuisha nguo za nyuzi zilizowakilisha upelekaji nje wa jumla ya 8.2% tu.

| | |
|---|---|
| | Sh. 800 na 1,200, lakini dengu ni Sh. 2,200 kwa kg);<br>• Hakuna vifaa vya kushughulikia uchafu; |

## 5. *Viwanda vya kukoboa, kusaga na kufungasha mchele na unga wa mahindi*

| Maelezo ya Fursa | |
|---|---|
| **Mambo Muhimu** | Uanzishaji wa viwanda vya uchakataji na ufungashaji wa mchele na unga wa mahindi huko Lamadi, Bariadi, Itilima, na Maswa. |
| **Mantiki ya uwekezaji huu** | • Kiasi cha uzalishaji wa mpunga na mahindi kinacho endelea kuongezeka;<br>• Kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa zilizochakatwa ambazo zimeimarishwa;<br>• Bei ndogo ya mazao wakati wa msimu wa uvunaji;<br>• Kushika masoko ya ndani na ya nje yenye mahitaji makubwa, hasa katika nchi jirani;<br>• Mahitaji makubwa ya bidhaa za mchele na mahindi katika nchi jirani. |
| **Msaada uliopo** | • Msaada mkubwa kutoka *PO-RALG*, *MALF*, *MITI*, na mamlaka za wilaya;<br>• Kuwepo kwa wanunuzi na walaji kwani watu wanaongezeka mkoani Simiyu kwa zaidi ya 2.8 % kwa mwaka;<br>• Ruzuku ya pembejeo inayotolewa na serikali kuu;<br>• Msaada kutoka katika vyama vya wakulima mf. Baraza la Mpunga Tanzania;<br>• Msaada wa kiufundi na kifedha kutoka *ASDP* II;<br>• Msaada kutoka kwa washirika wa maendeleo na watendaji wasio wa serikali. |
| **Changamoto/ Vihatarishi na hatua za kukabiliana nazo** | • Changamoto za hasara baada ya kuvuna, takriban 20-30%;<br>• Ubora wa ufungashaji na kuweka katika maghala kwa muda mrefu;<br>• Miundombinu ya hali ya chini ya mzunguko wa usambazaji;<br>• Uingiliaji wa makusudi wa kisiasa. |




*Mpunga na Mahindi*

## 6. *Vituo vya Mafunzo: Kituo kimoja cha mafunzo ya kilimo na mifugo Busega, na kituo kimoja cha mafunzo ya teknolojia ya viwanda Bariadi na Itilima, na Taasisi ya Mafunzo ya Afya Itilima*


| Maelezo ya Fursa | |
|---|---|
| **Mambo Muhimu** | 1. Uanzishaji wa shule maalum za sayansi za Sekondari za kidato cha kwanza hadi kidato cha sita katika wilaya zote, na matawi ya Taasisi za Teknolojia na Vyuo Vikuu vya Uhandisi katika wilaya zote<br>2. Uanzishaji wa kituo kimoja cha mafunzo ya kilimo na mifugo chenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 200 Busega<br>3. Uwekezaji katika Taasisi ya Mafunzo ya Afya Itilima,<br>4. Vyuo vya Mafunzo ya ualimu Zanzui na katika Halmashauri ya Itilima<br>5. Matawi ya Taasisi za Teknolojia na Vyuo Vikuu vya Uhandisi kwa ajili ya kupata vipaji na ujuzi wa hali ya juu huko Bariadi, Maswa, na Meatu. |
| **Mantiki ya uwekezaji huu** | • Rasilimali watu kuwa kitu muhimu katika maendeleo ya kilimo na viwanda mkoani Simiyu<br>• Uhaba wa nguvu kazi iliyo na utaalamu inaweza kukwamisha uwekezaji unohitaji maarifa muhimu mkoani Simiyu<br>• Zaidi ya wanafunzi 3,000 wa kidato cha nne na 1,000 wa ngazi ya kidato cha sita wapo katika shule zilizomo mkoani Simiyu;<br>• Uanzishaji wa mfumo wa elimu bure katika shule za msingi kuanzia Januari 2017 kutaongeza mahitaji ya mafunzo ya ufundi stadi katika muongo ujao;<br>• Maendeleo na kukua kwa technolojia na haja ya kuwa na rasilimali watu iliyo elimika na yenye ujuzi wa biashara na ufundi wa hali ya juu unaongeza haja ya kuwa na vyuo vya kuto mafunzo mkoani Simiyu<br>• Kiwango cha ongezeko la idadi kubwa ya watu cha 2.8 % huko Simiyu kinaongeza haja ya kuwa na vyuo vya kujengea uwezo wananchi. |
| **Msaada uliopo** | • Uwepo wa msaada wa uboreshaji wa elimu toka mamlaka za mikoa na wilaya;<br>• Msaada wa washirika wa maendeleo;<br>• Viwanda vinaweza kuwasaidia wafanyakazi wao kuongeza ujuzi. |
| **Changamoto/ Vihatarishi na hatua za kukabiliana nazo** | • Uwezo mdogo wa kulipia kozi za gharama kubwa;<br>• Michakato ya ukuzaji wa mitaala, usajili na utambuzi rasmi kuchukua muda mrefu;<br>• Kulinda viwango endelevu. |

## 7. *Viwanda vya uzalishaji na usafishaji wa mafuta ya mimea*

| Maelezo ya Fursa | |
|---|---|
| **Mambo Muhimu** | • Kuanzisha viwanda vya uzalishaji wa mafuta ya mimea na usafishaji Bariadi Vijijini na Itilima kutokana na mbegu za mafuta ya alizeti na pamba;<br>• Uzalishaji wa dizeli itokanayo na mimea/viumbe (*bio diesel*) kutokana na mafuta ya mbegu za pamba. |

| | |
|---|---|
| **Mantiki ya uwekezaji huu** | • Simiyu inazalisha kiasi kikibwa cha mbegu za alizeti, pamba na karanga;<br>• Tanzania ina pengo la zaidi ya tani 200,000 la mafuta ya mimea; Mafuta hayo huingizwa kutoka nje hususan Mashariki ya mbali;<br>• Mchakato wa ukamuaji na uchujaji unaotumika usio na ufanisi;<br>• Uhaba wa viwanda vya usafishaji mafuta;<br>• Mabaki ya mbegu yanahitajika kwa kiasi kikubwa kwa ajili ya chakula cha wanyama (Dola za Kimarekani 0.3 - 0.4 kwa kilo). |
| **Msaada uliopo** | • SIDO ina ujuzi wa kiasi kikubwa katika ujengaji wa uwezo wa wazalishaji na katika utengenezaji wa vifaa;<br>• Kuna idadi inayoongezeka ya wajasiriamali wachakataji ambao wanawekeza katika viwanda vidogo vya mafuta, ambavyo vinaweza kusaga zaidi ya mifuko 100 kwa siku kwa ufanisi;<br>• TIRDO inasaidia utafiti na maendeleo ya kiteknolojia;<br>• Kuna vyama vingi, AZISE na asasi za kiraia zinazosaidia uzalishaji wa mafuta ya mimea. Hizi zinajumuisha *Tanzanian Edible Oilseed Association (TEOSA)*, *Agricultural Marketing Cooperative Organizations (AMCOs)*, UMAMBE, *oil miller's association*, na Rural *Livelihood Development Company (RLDC)*. |
| **Changamoto/ Vihatarishi na hatua za kukabiliana nazo** | • Usambazaji wa kudumu wa mbegu bora za mafuta;<br>• Kukosekana kwa nishati ya umeme;<br>• Vifaa na teknolojia inayoingizwa kutoka nje ya nchi ni rahisi/haina gharama;<br>• Vifaa vinavyotumika katika usafishaji ni kutoka nje ya nchi tu;<br>• Uduni wa Miundombinu ya soko. |

## Mchoro wa 3.3: Uzalishaji wa alizeti katika wilaya ya Meatu katika msimu wa 2011/12-2015/16



*Kiasi kikubwa cha alizeti inayozalishwa kinaongezewa thamani nje ya mkoa na au nje ya nchi kwa sababu ya ukosefu wa viwanda vya kuchakata zao hilo. Wakulima Mkoani Simiyu hivi sasa wanatambua umuhimu wa kuzalisha alizeti na wanaongeza uzalishaji.*



*Shamba la Alizeti*

## 8. Huduma za tiba ya mifugo

| Maelezo ya Fursa | |
|---|---|
| **Mambo Muhimu** | • Uwekezaji katika huduma za tiba ya mifugo – hasa kliniki za tiba ya mifugo kwa ajili ya uchunguzi wa wanyama, tiba na chanjo;<br>• Kuanzisha huduma za uongeshaji katika majosho na tiba ya mifugo;<br>• Utengenezaji wa chanjo mbalimbali za mifugo Bariadi<br>• Uwepo wa eneo la uwekezaji Meatu, Maswa, Bariadi, Itilima, Busega. |
| **Mantiki ya uwekezaji huu** | • Simiyu ina ng'ombe zaidi ya milioni 1.5;<br>• Haja kubwa ya usambazaji wa dawa na chanjo mbalimbali (*Contagious Bovine Pleural (CBPP, Pneumonia), (FMD), Black Quarter (BQ), Newcastle disease, Anthrax, Black-quarter, Tick Borne diseases, and Brucellosis;*<br>• Haja ya maabara ya mifugo kwa ajili ya udhibiti wa magonjwa na usimamizi bora na salama wa bidhaa za mifugo. |
| **Msaada uliopo** | • Msaada wa kitaifa na wa serikali ya mtaa wa kiufundi, upanuzi, na kwa kiasi fulani wa kifedha;<br>• Kuendana na Dira ya Taifa 2025, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP II), Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP II) |

| | |
|---|---|
| **Changamoto/ Vihatarishi na hatua za kukabiliana nazo** | • Usambazaji na gharama za umeme;<br>• Uhaba wa vifaa vya ubaridi vya kuhifadhi chanjo na madawa |

## *9. Uanzishaji wa viwanda vya kusindika nyama ya ng'ombe na ya kuku*

Sekta ya mifugo katika Mkoa wa Simiyu inaweza kuongezeka mara tatu au zaidi kama yafuatayo yatatekelezwa: tafiti za kuboresha mifugo, kuongeza uzaishaji, na kuboresha mifugo kijenetiki; kupunguza viwango vya vifo vya mifugo kwa kuboresha upatikanaji wa huduma za tiba ya mifugo na uanzishaji wa kanda zisizo na magonjwa; uwekezaji katika uzalishaji na usambazaji wa chakula cha mifugo na mpango wa utumiaji wa ardhi ya malisho kwa ajili ya wafugaji; ukarabati sehemu za unywesheaji; uanzishaji wa masoko bora ya mifugo, machinjio, na mitambo ya ukamuaji maziwa na viwand vya kuongeza thamani.

| Maelezo ya Fursa | |
|---|---|
| **Mambo Muhimu** | Uanzishaji wa viwanda vya nyama ya ng'ombe, kwa kuanza na uwekezaji katika:<br>• Ongezeko la ranchi za ng'ombe wa kibiashara ili kuboresha kijenetiki (*genetic improvement*);<br>• Mashamba ya kunenepesha mifugo, na mashamba makubwa ya kibiashara ya mifugo kuhakikisha usambazaji wa kudumu wa ng'ombe bora;<br>• Uanzishaji wa uzalishaji wa chakula kisasa (*cattle fodder production*) na maghala yenye ubora<br>• Uanzishaji wa machinjio ya kisasa yenye majokofu yenye uwezo wa kuhifadhi ng'ombe kati ya 100 na 150 kwa siku. Ili kutoa nyama na bidhaa za nyama zenye ubora na salama kwa ajili ya walaji wa ndani na nje; na Mbuzi 50 kwa siku.<br>• Usambazaji wa vifaa vya machinjo;<br>• Viwanda vya kuweka nyama kwenye makopo;<br>• Uanzishaji wa mitambo mikubwa ya kushughulikia kuku kwa teknolojia ya kisasa;<br>• Mtambo kwa ajili ya kushughulikia na kuchakata mabaki ya wanyama waliochinjwa;<br>• Miradi ya uzalishaji na ufugaji bora. |
| **Mantiki ya uwekezaji huu** | • Simiyu ina zaidi ya makundi ya ng'ombe milioni 1.5 na kuku zaidi milioni 2.5;<br>• Watu wa Simiyu wanahitaji kufanya uwekezaji thabiti katika uzalishaji wa kibiashara wa kuku;<br>• Masoko ya uhakika katika nchi za Mashariki na Mashariki ya Kati, na Ulaya; |

| | |
|---|---|
| | • Ng'ombe wengi wa kiasili aina ya Zebu waliopo Simiyu. Zaidi ya 90% ya ng'ombe wanafugwa na wafugaji wadogowadogo na wafugaji wakulima, ambao mara nyingi wanakabiliwa na tatizo la uzalishaji mdogo na mavuno kidogo;<br>• Simiyu ina ikolojia inayofaa kwa kilimo, topografia, na ardhi ya malisho kwa ajili ya maendeleo ya ufugaji wa ng'ombe;<br>• Umuhimu wa kuboresha kijenetiki za ng'ombe wa kiasili na kuwa na mifugo iliyoboreshwa kwa uzalishaji mkubwa;<br>• Ongezeko la idadi ya watu, kukua kwa miji (urbanization) na kuongezeka kwa viwango vya mapato mkoani Simiyu vitaongeza mahitaji ya nyama katika miongo 2-3 ijayo;<br>• Machinjio mengi yaliyopo yana eneo dogo, ambalo linaweza kumudu uchinjaji wa ng'ombe kati ya mmoja na kumi kwa siku. Machinjio yana maeneo yasiyoendelezwa yaliyotengenezwa kwa ulingo wa saruji wenye paa la bati kwa ajili ya kivuli;<br>• Kuna masoko kwa ajili ya nyama ya ng'ombe yenye ubora ya Tanzania ambayo inakidhi viwango vya masoko ya ndani, kikanda, na ya nje mf. katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mashariki ya Kati, n.k.;<br>• Ongezeko la sasa la usambazaji wa mifugo nchini Tanzania (4-5%) linaweza lisifikie mahitaji ya baadaye hivyo uwekezaji mkubwa unahitajika mkoani Simiyu kutoa ujuzi wa kiufundi na mtaji wa kuendesha ranchi, sehemu za malisho, machinjio, vichakata nyama na uchunaji ngozi kulingana na ASDP II;<br>• Huduma za hali ya chini za msaada wa kiufundi na miundombinu ya masoko inatoa fursa nyingi za uwekezaji. |
| **Msaada uliopo** | • Simiyu imetambuliwa kitaifa katika *ASDP II* kwa ajili ya maendeleo ya viwanda vya nyama ya ng'ombe katika utaratibu mpya wa "Mkoa Mmoja Bidhaa Moja";<br>• Mamlaka za serikali zinazohamasisha Ushirikiano wa Sekta Binafsi na za Umma ili kuboresha mifumo ya usimamiaji na masoko ya ng'ombe;<br>• Uwepo wa Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo;<br>• Uwepo wa Taasisi ya Taifa ya Mifugo huko Mpwapwa;<br>• Serikali ya Tanzania inarekebisha uingizaji nchini usio wa haki wa bei ya nyama na bidhaa za nyama bandia;<br>• Serikali kuu inasaidia na kuhamasisha utafiti katika teknolojia ya nyama kuendana na mahitaji yanayoibuka;<br>• Mikopo inayofaa kutoka Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB), EADB, AfDB, n.k. |
| **Changamoto/ Vihatarishi na hatua za kukabiliana nazo** | • Baadhi ya watu wana zaidi ya ng'ombe 2000 ambao hawalishwi/ hawatunzwi ipasavyo;<br>• Wananchi wengi wana ardhi kubwa (Hekta 20-100) lakini hawatengi maeneo kwa ajili ya mashamba/ malisho, matokeo yake wamekuwa wakihamahama kutafuta malisho hata mikoa ya mbali, wakati mwingine kusababisha migogoro ya ardhi, uharibifu wa udongo na viumbe anuwai, na kuingia kinyume cha sheria katika hifadhi za wanyama;<br>• Ng'ombe wa wastani ana uzito wa chini wa kg 200, jambo ambalo linafanya wafugaji wapate bei ya chini ya Sh. 200, 000 mpaka sh. 300,000. Ng'ombe aliyelishwa vizuri anauzwa Sh. 700,000 mpaka Milioni 1 mnadani; |

| | |
|---|---|
| | • Wazalishaji nyama ya ng'ombe na vyama vya wafanyabiashara visivyo na nguvu;<br>• Changamoto za usafi na ubora wa sehemu za kufugia;<br>• Haja ya kuweka utambulisho wa mifugo, mfumo wa kuweka kumbukumbu na mfumo wa ufuatiliaji kwa ajili ya uzalishaji salama na wenye ubora wa nyama;<br>• Ushindani usio wa haki kutoka katika nchi nyingine, mf., Brazil na Umoja wa Ulaya, hasa Mkataba wa Ushirikiano wa Kiuchumi (EPA) kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya ambao unawapa Umoja wa Ulaya kuingiza bidhaa za nyama ya ng'ombe ya Umoja wa Ulaya katika soko la Tanzania nyama bila kutozwa ushuru;<br>• Upatikanaji wa maji ya kutosha. |

## *10. Viwanda vya ngozi*

| Maelezo ya Fursa | |
|---|---|
| **Mambo Muhimu** | Uanzishaji wa viwanda vya ngozi vyenye teknolojia rafiki kwa mazingira na michakato ya kikemikali na kimakanika (*mechanical*) na uhifadhi wa ubora. |
| **Mantiki ya uwekezaji huu** | • Upataji na usambazaji mkubwa wa malighafi. Simiyu ina zaidi ya ng'ombe milioni 1.5, mbuzi 700,000, na kondoo 300,000;<br>• Upataji wa teknolojia ya uchakataji na vifaa;<br>• Kiasi kidogo cha nguvu kazi na gharama za kazi;<br>• Soko la ndani linalokua, kama ilivyoonyeshwa katika maonyesho ya biashara ya Nane Nane na Saba Saba;<br>• Upataji wa masoko ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, SADC na Umoja wa Ulaya;<br>• Sera zinazosaidia za serikali kuu na za wilaya. |
| **Msaada uliopo** | • Misaada ya kitaasisi, kiufundi na kifedhaa inayotolewa na VETA, DIT, MALF, MITI, TIRDO, SIDO, Magereza, JKT Suma, na AZISE<br>• Kuendana na Dira ya Taifa 2025, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP II), Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP II) |
| **Changamoto/ Vihatarishi na hatua za kukabiliana nazo** | • Uendeshaji wa machinjio unapaswa kuwa wa kitaalamu na wa kisasa;<br>• Kupata ngozi yenye uzito mkbwa zaidi ya kg 10 ni changamoto;<br>• Ng'ombe wanachinjwa wakiwa wamezeeka, zaidi ya miaka 4;<br>• Mchakato wa taratibu wa kuelekea utendaji wa kisasa na wafanyakazi wenye mafunzo wasiotosheleza vinakwamisha utendaji wa viwanda vya ngozi;<br>• Uwezo mdogo wa maendeleo ya soko la viwanda vya ngozi na watengenezaji wa bidhaa za ngozi;<br>• Utumiaji wa maji na uchafuzi wa maji ni changamoto kubwa katika tasnia ya ngozi; kunaweza kuwa na ugumu katika utekelezaji unaofaa wa mfumo wa sera ya Mazingira ya 2017;<br>• Haja ya kuboresha utafiti, uvumbuzi na teknolojia, kuboresha mbinu za uchinjaji, na kuboresha usimamizi wa mazingira. |

| | |
|---|---|
| | • Uwekaji alama wa kiasili /duni (pamoja na upigaji viboko mifugo) kwenye ngozi ya wanyama unaathiri bidhaa za ngozi. |



*Ng'ombe katika wilaya ya Meatu*

## 11. Viwanda vya uzalishaji bidhaa za ngozi

| Maelezo ya Fursa | |
|---|---|
| **Mambo Muhimu** | • Viwanda vya uzalishaji wa bidhaa bora za ngozi huko Meatu, Itilima, Bariadi na Maswa;<br>• Uanzishaji wa pamoja wa uzalishaji wa bidhaa za ngozi (*leather goods cluster*). |
| **Mantiki ya uwekezaji huu** | • Simiyu inatoa kiasi cha ngozi 40,000 za ng'ombe, mbuzi na kondoo;<br>• Ngozi nyingi zinauzwa nje ya mkoa nje ya mkoa au kusafirshwa nje ya nchi, mf. kwenda Kenya, India, n.k.;<br>• Ingawa kuna wajasiriamali wanazitumia ngozi ndani ya nchi, bado kiasi kikubwa cha ngozi kinapelekwa nje ya nchi;<br>• Eneo muhimu kwa uzalishaji, uuzaji na usafirishaji nje wa mikoba, viatu, soli yenye ngozi, nguo, vikorokoro vya nguo za ngozi, na samani;<br>• Uwezo mdogo wa kukamilisha mzunguko wa thamani wa ngozi za Simiyu na Tanzania;<br>• Kutokana na kukua kwa daraja la kati (middle class) kuna umuhimu wa kuzalisha kwa ajili ya soko la walaji wa bidhaa kama vile mikoba, viatu, makoti, na samani; |
| **Msaada uliopo** | • Msaada wa serikali unaotoa mafunzo kwa wataalam wa ngozi mf. 2017 unatoa nafasi 1,000 DIT Mwanza. |


| | |
|---|---|
| **Changamoto/ Vihatarishi na hatua za kukabiliana nazo** | • Hali ya misimu: Wakati mwingine kunaweza kusiwe na ngozi bora kwa ajili ya viwanda vya ngozi;<br>• Ubora wa ngozi unaoathiriwa na viboko na uwekaji alama katika mifugo;<br>• Kukosekana huduma za uhakika za kifedha<br>• Ubora wa ngozi ya mifugo unaoathiriwa na uuzaji wa mifugo wakiwa wazee au wagonjwa (zaidi ya miaka 5);<br>• Ushindani kutoka ngozi sanisi na bidhaa sanisi (*synthetic leather*). |

## 12. Viwanda vya bidhaa za maziwa

| Maelezo ya Fursa | |
|---|---|
| **Mambo Muhimu** | • Uanzishaji wa viwanda vya uchakataji maziwa na bidhaa za maziwa;<br>• Kuwekeza katika uzao ili kupata ng'ombe chotara wenye mavuno mengi na wanaohimili magonjwa;<br>• Kuwekeza katika ranchi ndogo na ranchi kubwa;<br>• Uanzishaji wa mashamba ya ng'ombe wanaolishwa nyumbani;<br>• Maeneo ya uwekezaji: Maswa, Bariadi, Itilima. |
| **Mantiki ya uwekezaji huu** | • Simiyu ina ng'ombe zaidi ya milioni 1.5;<br>• Uzalishaji wa maziwa uko mikononi mwa wamiliki wadogo wadogo; wazalishaji wakubwa ni wachache;<br>• Maziwa ni mengi kuanzia Novemba mpaka Aprili;<br>• Masoko yapo ndani ya Wilaya na Halmashauri ya Mji wa Bariadi, Lamadi, Mwanza, na mahoteli;<br>• Bei ndogo ya maziwa ya shambani, Sh. 400 kwa lita, wakati mtindi una gharama ya zaidi ya Sh. 4,000/L (Bei ya maziwa ya Meatu);<br>• Uchakataji maziwa unafanywa kienyeji katika ngazi za kaya na kijiji kwa kuhusisha vitengo vidogo vidogo vya uchakataji visivyosajiliwa;<br>• Nyongeza ya thamani kuimarisha usalama wa chakula na lishe, kupunguza umaskini wa kipato, na kuboresha viwango vya maisha ya wafugaji;<br>• Pengo kubwa upatikanaji wa bidhaa za maziwa zilizongezwa thamani katika soko la Simiyu;<br>• Utamaduni na uwezo wa watu (pato la mtu Dola za Kimarekani 250) linaruhusu unywaji wa mara kwa mara wa maziwa. |
| **Msaada uliopo** | • Uwepo wa Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo;<br>• Msaada wa kisiasa wa mamlaka za wilaya na ugharimiaji wa Mipango ya Mandeleo ya Wilaya. |
| **Changamoto/ Vihatarishi na hatua za kukabiliana nazo** | • Changamoto zaujazo (kiasi kisichofaa);<br>• Changamoto za usafirishaji – vituo vya ukusanyaji mpaka katika mitambo ya uchakataji; ukosefu wa majokofu;<br>• Uhaba wa maziwa msimu wa ukame Mei-Julai kwa sababu ya changamoto za maji na malisho; |

| | |
|---|---|
| | • Kiasi kikubwa cha gharama za uzalishaji kinachohusishwa na taratibu za leseni, gharama za huduma na gharama zisizo rasmi;<br>• Tofauti kubwa ya kimisimu;<br>• Haja ya kuwekeza katika ununuzi wa ng'ombe wanaotoa maziwa mengi; |

**Maziwa ya mgando yanayozalishwa na kundi la vijana Meatu, mkoani Simiyu**




*Mtindi unaozalishwa na kikundi cha vijana wa meatu*

## 13. Usambazaji wa umeme

| Maelezo ya Fursa | |
|---|---|
| **Mambo Muhimu** | • Njia ya usambazaji wa umeme 400-500 MW kutoka katika gridi ya taifa kufika mwaka 2050;<br>• Uzallishaji wa umeme kutokana na biogesi ya uchafu wa mazao na mifugo, na umeme wa jua (photovoltaic panel) (>50 KVA) |
| **Mantiki ya uwekezaji huu** | • Usambazaji wa kutosha wa nishati utahitajika kwa ajili ya kuendesha mifumo ya umwagiliaji, Viwanda, na matumizi ya nyumbani kwa idadi watu inayokua haraka na uhamiaji wa watu wanaotafuta ajira mkoani Simiyu;<br>• Simiyu ina ng'ombe zaidi ya milioni 1.5, ambao kinyesi chao kinaweza kutumiwa kwa urahisi kwa uzalishaji wa biogesi;<br>• Simiyu ina masaa 11 ya jua kali karibu mwaka mzima linalotoa fursa kubwa kwa ajili ya uzalishaji wa kiuchumi wa umeme wa PV wa majumbani, kuendesha mifumo ya umwagiliaji, na mtambo wa umeme wa viwandani;<br>• Muhimu kwa ajili ya kuwezesha jumuiya za vijijini zisizo na gridi na viwanda vya vijijini kwa kuhamasisha nishati iliyopelekwa vijijini na vyanzo vya ndani vya nishati jadidifu. |

| | |
|---|---|
| **Msaada uliopo** | • Misaada kutoka MEM, CoET-UDSM, TIRDO, TANESCO, REA, WBU, watu binafsi, UNIDO, GEF, UNDP, Kituo cha Afrika Mashariki cha Nishati Jadidifu na Ufanisi wa Nishati ( *East African Centre for Renewable Energy and Energy Efficiency) (EAC-REEE)*, Mfuko wa Changamoto za Viwanda Afrika *(Africa Enterprise Challenge Fund)*, n.k;<br>• Msaada thabiti kutoka kwa watoaji wa mifumo ya nishati ya jua;<br>• Sera na msaada wa kiufundi kutoka serikalini na washirika wa maendeleo, na nishati ya jua na biashara ambazo hazimo katika gridi. |
| **Changamoto/ Vihatarishi na hatua za kukabiliana nazo** | • Mtaji mkubwa;<br>• Ujengaji uwezo wa mwanzo unahitajika;<br>• Gharama za juu za kuanzisha mradi na muendelezo wake. |

## *14. Maeneo Matatu ya Viwanda (Industrial Parks)*

| Maelezo ya Fursa | |
|---|---|
| **Mambo Muhimu** | Uanzishaji wa maeneo matatu makubwa na muhimu ya viwanda, Lamadi - Bariadi (50km x 60km), Maswa - Malampaka, (30km x 30km) ; Mwandoya - Ngh'oboko, (30km x 30km) Meatu; Lagangabilili - Lugulu, (15km x 15km) Itilima; na kituo cha uzalishaji wa bidhaa za mauzo ya nje (export processing facity) Malampaka Maswa.<br>Kwa kuanzia, Maeneo ya viwanda yatajumuisha fursa zifuatazo za uwekezaji katika namna ya makundi, viwanda, na vituo vya huduma:<br>1. Kundi la utengenezaji:<br>a. Vinu vya kuchambulia pamba;<br>b. Viwanda vya nguo na mavazi;<br>c. Pamba iliyoongezwa thamani - kwa viwanda vya bidhaa;<br>d. Machinjio, Nyama ya Ng'ombe na ya Kondoo;<br>e. Uchakataji na ufungashaji wa nafaka;<br>f. Kiwanda cha bidhaa za nyama;<br>g. Viwanda vya ngozi (vitengo vya ukamilishaji wa uzalishaji wa ngozi, uzalishaji wa bidhaa za ngozi);<br>h. Viwanda vya kuongeza thamani ya mazo ya kilimo (Viwanda kwa ajili ya uchakataji na uwekaji katika makopo bidhaa za chakula, viwanda vya bidhaa za maziwa, viwanda vya mbegu za mafuta-hasa vya mafuta ya mimea na usafishaji, chakula cha mifugo, na vinywaji);<br>i. Kituo cha huduma na maelezo;<br>j. Kituo cha maghala;<br>k. Kituo cha huduma za umma; Kituo cha kikubwa cha mafuta;<br>l. Kituo cha kushughulika uchafu utokao viwandani;<br>m. Mitambo ya malighafi za viwandani<br>2. Kituo cha Huduma za Uchumi na Biashara: Kituo cha Biashara, Kituo cha Fedha na Bima; Kituo cha Biashara cha ubadilishanaji bidhaa za kilimo; na Kituo cha Usambazaji wa Huduma; |

| | |
|---|---|
| | 3. Kundi la Huduma za Jamii: Vituo vya Abiria na usafirishaji; vituo vya ustawi; vituo vya mafunzo; na maduka makubwa;<br>4. Kundi la Uunganishaji: Uunganishaji, ufungashaji, na uongezaji thamani katika mashine, vifaa, na bidhaa nyingine za viwanda, mf. mashine na zana za viwandani, vifaa vya machinjio n.k.;<br>5. Tasnia ya ukarimu (mahoteli, migahawa, burudani, utalii)<br>6. Vituo vya Masoko: Ubadilishanaji wa Bidhaa za Kilimo huko Lamadi, masoko ya kisasa Bariadi na Maswa; na Kituo kimoja cha Soko/Mnada wa Mifugo huko Meatu;<br>7. Mashamba ya Misitu na Matunda (mf., miombo, seda, mikalitusi ya kisasa, fito) kuhakikisha ubora wa hewa, mbao, mbao za vibanzi, tabaka la mbao, bamba la nyuzi, samani, boriti, ufugaji wa nyuki, na usalama wa lishe;<br>8. Makundi ya teknolojia ya juu<br>9. Uzalishaji wa nishati, biogesi, photovoltaic solar panels, uzalishaji wa makaa, kiwanda cha mvuke<br>10. Vituo vya burudani;<br>11. Ufungashaji na usambazaji; |
| **Mantiki ya uwekezaji huu** | • Maendeleo endelevu yaliyofikiriwa vizuri, yaliyoundwa na kupangwa kwa pamoja kwa ajili ya maendeleo endelevu ya mkoa wa Simiyu;<br>• Haja ya uwekezaji wa umma na binafsi katika upangaji wa miji na maendeleo ya miundombinu ya miji ili kuwa na miji iliyopangwa vizuri kwa kuzingatia sheria na kanuni;<br>• Simiyu iko kimkakati kwa uwekezeja katika maeneo ya viwanda. Ina fikika kwa urahisi kutokea pande zote za biashara ya EAC na COMESA kwa njia ya ardhi na njia za majini;<br>• Muunganiko mzuri katika bandari za Ziwa Victoria, Kiwanja cha ndege cha Mwanza. Reli ya Kati inatoa muunganiko katika bandari kuu ya Dar es Salaam na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, ambao unatoa hakikisho la usafirishaji wa bidhaa kwa anga na majini kutoka na kwenda katika masoko ya kimataifa. Reli kutoka Mwanza - Dar es Salaam na Barabara ya Tunduma na reli ya TAZARA inatoa muunganiko na Kusini mwa Tanzania na nchi za SADC;<br>• Eneo la uwekezaji wa muda mrefu kwa miundombinu ya kiumbo na kiufundi. |
| **Msaada uliopo** | • Msaada mkubwa wa taifa na nchi za ukanda.<br>• Serikali kuu ina mpango wa kujenga uwanja wa ndege huko Igegu, Bariadi |
| **Changamoto/ Vihatarishi na hatua za kukabiliana nazo** | • Upatikanaji wa fedha;<br>• Changamoto za usafirishaji, nishati, huduma za umma, na rasilimali watu wenyeujuzi;<br>• Ukosefu wa makundi ya viwanda yenye ufanisi kuimarisha ubora na uvumbuzi;<br>• Msaada madhubuti, wa ubunifu, na endelevu wa serikali na sekta binafsi unahitajika;<br>• Uratibu mbovu wa waendeshaji wa biashara katika mzunguko wa thamani unaweza kusababisha maendeleo ya mgawanyiko;<br>• Haja ya awali ya kufanya upimaji wa ardhi wa kina kwa ajili ya kuweka mipaka ya ardhi na utaratibu wa mipango ya matumizi ya ardhi. |

## 15. *Eneo la makazi: Ujenzi wa nyumba bora na nafuu na maduka makubwa, na vyumba vya mikutano na ofisi kwa ajili ya ukodishaji.*

| Maelezo ya Fursa | |
|---|---|
| **Mambo Muhimu** | • Ujenzi wa nyumba za mita za mraba 60-120 ndani ya kiwango cha bei cha Sh. Milioni 25 - 50, kutegemea na eneo, ubora, upataji wa vifaa vya ujenzi na mahitaji mengine;<br>• Nyumba 5,000 mpaka 10,000 kufikia mwaka 2040;<br>• Maduka makubwa,<br>• Vyumba vya mikutano na ofisi kwa ajili ya ukodishaji. |
| **Mantiki ya uwekezaji huu** | • Zaidi ya 40% ya wakazi wa Simiyu wana umri chini ya miaka 30 na watahitaji nyumba katika muongo ujao;<br>• Simiyu ni mkoa mpya. Kutakuwa na ongezeko la wahamiaji katika maeneo ya miji ya katikati pamoja na wafanyakazi wa serikali;<br>• Idadi kubwa ya watu katika miji inayokua haraka wanahitaji nyumba za kisasa za makazi na maduka makubwa, na huduma za ofisi za biashara;<br>• Mwekezaji yeyote mtarajiwa mwenye mtaji anakaribishwa kuja kuwekeza katika maeneo ya makazi katika halmashauri zote za wilaya mkoani Simiyu;<br>• Kiwango cha uongezeko la watu cha 2.8% mkoani Simiyu kitasababisha mahitaji yasiyopungua ya nyumba. |
| **Msaada uliopo** | • Msaada uliopo wa kuboresha elimu kutoka mamlaka za mkoa na wilaya;<br>• Msaada wa taasisi za kifedha;<br>• TBA na SUMA JKT, Shirika la Nyumba la Taifa wanaweza kujenga nyumba nafuu kulingana na mahitaji maalum ya ndani;<br>• Mashirika ya ujenzi yanayoshindana ya ndani na ya kigeni yanapandisha viwango vya ubora. |
| **Changamoto/ Vihatarishi na hatua za kukabiliana nazo** | • Uhaba wa huduma za uwekaji rehani;<br>• Viwango vya juu vya taasisi vinazokopesha kwa ajili ya maendeleo ya makazi;<br>• Changamoto muhimu pamoja na huduma za msingi. |

## 16. *Vitalu vya uwindaji na Makambi katika Hifadhi ya Wanyama ya Maswa na Eneo la Usimamizi wa Wanyama la Makao*

| Maelezo ya Fursa | |
|---|---|
| **Mambo Muhimu** | • Uanzishaji wa maeneo ya makambi katika hifadhi ya wanyamapori ya Maswa, ambayo ina km za mraba 2,880 na Eneo la Usimamizi wa Hifadhi ya Wanyamapori ya Makao (km za mraba 1,330) katika wilaya ya in Meatu;<br>• Uanzishaji wa hoteli za nyota 2-3<br>• Uanzishaji na uhifadhi wa vitalu vya uwindaji katika hifadhi ya wanyama ya Maswa na eneo la usimamizi wa wanyamapori la Makao; |

| | |
|---|---|
| | • Uanzishaji wa uendeshaji wa utalii wa utamaduni katika maeneo ya utamaduni hai ya Hadzabe, Sukuma na mfuko wa Taturu huko Maswa, Wilaya za Meatu, Busega, Itilima na Bariadi Vijijini.<br>• Uanzishaji wa ushughuli za kitalii;<br>• Uendelezaji wa hifadhi za misitu huko Maswa. |
| **Mantiki ya uwekezaji huu** | • Hifadhi ina wanyamapori mbalimbali kama vile simba, kiboko, nyati, pundamilia, mbwamwitu, mbawala, swalapala, twiga na nyani;<br>• Utalii unaweza kuunda kwa urahisi maelfu ya kazi katika ngazi ndogo ya ujuzi iliyowekwa ndani ya mwelekeo wa sekta ya utalii, na sio moja kwa moja katika pande nyingine ikiwa ni pamoja na kilimo, uchakataji wa mazao ya kilimo, miundombinu na anga;<br>• Uanuwai wa uoto na mimea;<br>• Ukuzaji wa ziara za kitalii;<br>• Tasnia ya ukarimu iliyodunishwa. |
| **Msaada uliopo** | • Msaada wa kiuendeshaji kutoka Bodi ya Utalii Tanzania, Bodi ya Leseni za Utalii;<br>• Msaada wa sera kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii;<br>• Msaada kutoka vyama vya utalii, mf. Chama cha Mahoteli Tanzania (Simu. +255 (0)22 2602440 www.hat-tz.org / info@hat-tz.org), n.k. |
| **Changamoto/ Vihatarishi na hatua za kukabiliana nazo** | • Mnamo mwaka 2011, Tanzania ilikuwa ya 110 kati ya nchi 139 katika sekta ya ushindani wa kiutalii, licha ya kushika nafasi ya pili duniani kwa majaaliwa ya rasilimali zetu;<br>• Changamoto zinazoidhinisha utendaji zinajumuisha udhibiti uliozidi na mahitaji ya kifedha ambayo huufanya kuwa mgumu kwa uendeshaji wa nchi kushiriki katika soko;<br>• Haja ya kuhamasisha maendeleo ya mtangamano wa soko la sekta ya utalii katika Mkoa wa Simiyu;<br>• Haja ya kuunda biashara ya kirafiki zaidi ya sekta ya uwekezaji kwa kuanza na uhakiki wa sera na Sheria;<br>• Kuongeza ushiriki wa mdau katika mzunguko wa thamani wa uongozi kuimarisha utendaji katika Mkoa wa Simiyu; na<br>• Kuchapuza marekebisho ya kuimarisha ukuaji wa sekta ya utalii ili iweze kuwa miongoni mwa makusudio kumi ya juu barani Afrika. |



*Hifadhi ya misitu*

## 17. Teknolojia kwa uhifadhi wa muda mrefu wa mazao ya shamba, mifugo, na bidhaa za baharini

| Maelezo ya Fursa | |
|---|---|
| **Mambo Muhimu** | Kuwekeza katika teknolojia kwa uhifadhi wa muda mrefu waa mazao ya shamba, mifugo na bidhaa za samaki<br>• Tani za mita 1,000-5,000 za mabohari katika ngazi ya kijiji;<br>• Mabohari ya tani 5,000- 50,000 ya Mpunga Malampaka namahindi huko Itilima;<br>• Tani 50-200 za nyama zinazohifadhiwa katika ubaridi huko Meatu na Maswa;<br>• Tani 10-50 za uhifadhi wa baridi wa bidhaa za samaki huko Busega. |
| **Mantiki ya uwekezaji huu** | • Hasara kubwa ya uvunaji, ca. 20-30%<br>• Uhaba wa nafasi ya kuhifadhia, hasa wakati wa mavuno mengi, mfano katika miaka ya 2013-2015;<br>• Uwezo mdogo wa Wakala wa Hifadhi ya Akiba ya Chakula (tani 250,000 tu). |
| **Msaada uliopo** | • Kuwepo kwa msaada kutoka serikali kuu, mamlaka za mkoa na wilaya;<br>• Msaada wa taasisi za kifedha na washirika wa maendeleo mfano, USAID, Benki ya Dunia, AfDB, n.k.<br>• Usafirishaji mzuri nje wa vyakula na mazao ya chakula kuhakikisha maingizo katika uwekezaji |
| **Changamoto/ Vihatarishi na hatua za kukabiliana nazo** | • Upataji wa mtaji kwa ajili ya ujenzi, uendeshaji, na utengenezaji<br>• Changamoto muhimu ndani ya huduma za umma;<br>• Ushughulikiaji wa changamoto za utunzaji wa vijito vya maji machafu na mazingira kama hayo;<br>• Utumiaji wa vitu visivyofaa (mfano. zebaki) na njia kwa uziduaji kwa wachimbaji wadogowadogo. |

## 18. Ufugaji wa Samaki kwa Kutumia Vizimba na Matanki (RAS)

| Maelezo ya Fursa | |
|---|---|
| **Mambo muhimu** | • Ufugaji wa samaki kwa Kutumia Vizimba na Matanki (RAS)<br>• Kuendesha utafiti endelevu kubainisha maeneo kwa uwekezaji wa vizimba<br>• Kuanzisha sehemu kwa ajili ya uanguajisamaki wadogo wa kufuga.<br>• Uanzishaji wa viwanda vya uchakataji wa chakula cha samaki<br>• Ujengaji wa hifadhi baridi na maeneo ya maonyesho/mfano (sites)<br>• Mtambo/kiwanda cha kuchakata samaki<br>• Maeneo kwa ajili ya uwekezaji: Katika Halmashauri ya Bariadi mjini, Busega na Bariadi. |
| **Mantiki ya uwekezaji huu** | • Simiyu ina eneo la zaidi ya kilometa za mraba 605 na kilometa 78 za ufuko katika Ziwa Viktoria;<br>• Samaki katika vyanzo vya uvuaji katika ziwa Victoria wanapungua kwa kasi;<br>• Hisia za uwekezaji zitaongeza uzalishaji wa samaki kwa masoko ya kitaifa na kimataifa;<br>• (Ufugaji wa samaki kupunguza mfumo wa ikolojia wa Ziwa Viktoria unafifishwa na uvuvi haramu;)? |

| | |
|---|---|
| | • Kuongeza shughuli za ufugaji wa samaki kutavutia wawekezaji kujenga masoko ya kisasa ya samaki na vifaa vya uchakataji wa samaki katika Halmashauri ya Wilaya ya Busega;<br>• Watu wa Simiyu na maeneo ya jirani kwa kawaida wanatumia samaki kama chanzo cha protini<br>• Kuwepo kwa Masoko ya kutumainiwa nchini na nje ya nchi<br>• Chanzo cha protini kilichopendekezwa badala ya nyama nyekundu<br>• Pato la taifa (Dola za Kimarekani 250) kuruhusu ulaji wa mara kwa mara wa samaki |
| **Msaada uliopo** | • Sera na mkakati wa taifa wa Uvuvi;<br>• Msaada wa kisiasa wa taifa, mamlaka za kimkoa na usaidizi wa kifedha wa mpango wa maendeleo ya wilaya<br>• Kuwepo karibu kwa miradi ya mfano |
| **Changamoto/ Vihatarishi na hatua za kukabiliana nazo** | • Ukosefu wa mzalishaji wa kuaminika wa kuangua samaki wadogo wa kufuga (fingerlings)<br>• Ukosefu wa vituo vya ukusanyaji katika mitambo ya kuchakata.;<br>• Ukosefu wa chakula cha kutumainiwa cha samaki na bei ya juu ya chakula cha samaki cha kutoka nje<br>• Haja ya kuwekeza katika jitihada za ununuaji kwa vizimba na Katibu Mkuu wa Mkoa |



*Ufugaji wa samaki katika vizimba na matanki*

## 19. Uchunguzi wa rasilimali ya madini, uyeyushaji madini, usafishaji wa nikeli, chumvi, kokoto na jasi

| Maelezo ya Fursa | |
|---|---|
| **Mambo muhimu** | • Uchunguzi wa rasilimali ya madini, uyeyushaji, usafishaji wa nikeli na dhahabu muhimu, mawe ya madini, shaba,<br>• Madini, ushughulikiaji na biashara ya almasi, chumvi, bidhaa za machimbo, na jasi;<br>• Teknolojia kwa ajili ya uchunguzi wa madini, |

| | |
|---|---|
| **Mantiki ya uwekezaji huu** | • Madini yapo mkoani Simiyu<br>• Madini mengi yako chini ya uchimbaji mdogo unaotumia teknolojia ya chini. Teknolojia ya kisasa ingeboresha mavuno yao;<br>• Soko la nyumbani na la kimataifa lililopo kwa ajili ya malighafi ambalo linakidhi viwango vya kimataifa; |
| **Msaada uliopo** | • Kuwepo kwa msaada kutoka serikali kuu, mamlaka za mkoa na wilaya;<br>• Msaada kutoka katika taasisi za fedha na vyama vya madini;<br>• Usafirishaji nje ulio bora; |
| **Changamoto/ Vihatarishi na hatua za kukabiliana nazo** | • Upatikanaji wa wafanyakazi na wachimbaji wenye ujuzi;<br>• Utaalamu wa kutibu maji taka yatokayo katika migodi na utunzaji wa mazingira. Utumiaji wa kemikali zenye madhara (mf. zebaki) na njia hatarishi zitumiwazo na wachimbaji wadogowadogo. |







*Chaki bora inayozalishwa na kikundi cha vijana wa Maswa*

## 20. Ujenzi wa gati na kituo cha burudani Nyamikoma, usafiri wa majini, kuangalia ndege wanaoishi kwenye maji, kupiga mbizi ndani ya maji ya kina kirefu, michezo ya kuvua samaki na ujenzi wa kituo cha michezo ya ndani ya maji wilayani Busega. ufukwe wa km 78

| Maelezo ya Fursa | |
|---|---|
| **Mambo muhimu** | Uanzishaji wa bandari Nyamikoma, na Vituo vya Burudani utazamaji wa mzunguko wa maji na ndege katika Ziwa Viktoria katika Halmashauri ya Wilaya ya Busega ufukwe wa km 78 |
| **Mantiki ya uwekezaji huu** | • Umuhimu na matumizi madogo ya vivutio vya asili vya utalii;<br>• Vifaa vilivyopo havitoshi kukidhi mahitaji ya idadi inayoongezeka ya watalii wa ndani na wa nje;<br>• Kuongeza uelewa wa Watanzania katika vivutio vya utalii wa ndani na umuhimu wake katika kujifunza na kupumzika.<br>• Haja ya kuboresha huduma kufikia viwango vya kimataifa. |

| | |
|---|---|
| **Msaada uliopo** | Msaada imara wa kiufundi kutoka Bodi ya Utalii Tanzania, Mamlaka za Mikoa, na Wizara ya Maliasili na Utalii. |
| **Changamoto/ Vihatarishi na hatua za kukabiliana nazo** | • Usimamizi wa fedha;<br>• Utaalamu wa kiufundi. |

## 3.3 Makundi yanayolengwa na Mwongozo huu

Wanufaika wa moja kwa moja wanaolengwa na Mwongozo huu ni;

- Wawekezaji, wamiliki wa biashara, wamiliki wa makampuni yanayoendesha mashamba makubwa ya mazao ya kilimo na makampuni ya uongezaji thamani ya mazao na masoko yanayokusudia kuwekeza katika maeneo ya viwanda na biashara yaliyotengwa katika mkoa wa Simiyu;
- Wizara ya Biashara, Viwanda na Uwekezaji;
- Wadau mbalimbali katika mnyororo wa thamani, ikiwa ni pamoja na wajasiriamali binafsi, waingizaji na wasafirishaji nje wa pembejeo na mazao ya kilimo, wafugaji wa mifugo na wavuvi kwa ujumla. Asasi za viwanda/bodi za mazao na masoko.;
- Wizara za serikali, wakala, Mamlaka za Serikali za Mitaa, EPZA, na mashirika ya umma (mf. yale yanayowajibika na kilimo, viwanda, biashara, fedha, na ushirikiano wa kimataifa);
- Vyombo vingine vya sekta binafsi;
- Wanataaluma/watafiti katika Ukanda wa Ziwa na nchini Tanzania;
- Asasi za Ufadhili kama vile Baraza la Taifa la Biashara, TCCIA, mifuko ya pensheni inayowekeza katika kilimo na viwanda, na taasisi nyingine za misaada;
- Taasisi zinazosimamia usimamizi wa ubora na masuala ya usimamizi wa usalama, kama vile TBS, TFDA n.k;
- Asasi zinazotoa uwezo wa uzalishaji, habari na data, Ufuatiliaji na Tathmini (M&E), na huduma nyingine za kusaidia biashara, mashirika ya Kusaidia Viwanda (ISOs), Kitengo cha Maendeleo ya Utengenezaji wa Nguo, BRELA, TRA, FCC, NEEC, TANTRADE, n.k.;
- Asasi za kijamii na asasi zisizo za kiserikali; na
- Washirika wa Maendeleo, kama FAO, UNDP, Benki ya Dunia, UNCTAD, ITC, EU, UNIDO, TMEA, n.k.

Sehemu ya nne:

# UWEZESHAJI, MICHAKATO, MAHITAJI NA MOTISHA

## 4.1 Uwezeshaji

Mkoa wa Simiyu na Serikali Kuu zinaboresha mazingira yanayofaa ili kushawishi na kuwezesha uwekezaji katika Mkoa wa Simiyu katika maeneo yaliyoonyeshwa katika sehemu ya tatu ya Mwongozo huu. Sera, sheria, mikakati, mipango na programu kuu za uwekezaji ambazo zinahamasisha uwekezaji katika wilaya zimeonyeshwa hapo chini.

***Mazingatio ya Sera, Sheria, Taasisi na Udhibiti:***

***Sera Kuu:***

Sera zinazoongoza uhamasishaji uwekezaji katika Mkoa wa Simiyu zinajumuisha: Sera ya Taifa ya Uhamasishaji wa Uwekezaji, 1996, Sera ya Taifa ya Kilimo 2013, Sera ya Taifa ya Mifugo 2006, Sera ya Taifa ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda (SIDP) 1996-2020, Sera ya Taifa ya Biashara kwa Uchumi wa Ushindani na Kuelekea Ukuaji wa Biashara ya Nje, Sera ya Taifa ya Shughuli Ndogo za Kifedha, 2015, Sera ya Taifa ya Misitu (1998), Sera ya Ufugaji wa Nyuki (1998), Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na vya Kati (2003), Sera ya Taifa ya Ardhi (1995), rasimu ya Sera ya Taifa ya Mazingira 2016, Sera ya Madini ya Tanzania, (2009), Mwongozo wa Mwekezaji wa Tasnia ya Madini Tanzania, 2015, na Dira ya Mkoa wa Simiyu na sera za maendeleo.

***Mfumo wa kisheria:***

Sheria kuu na kanuni ambazo zinaongoza uhamasishaji wa uwekezaji na shughuli katika Mkoa wa Simiyu ni: Sheria ya uwekezaji Tanzania (1997), Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania 2006, Sheria ya Ardhi (1999), Sheria ya Ardhi ya Vijiji (1999), Sheria ya Madini (1998), Sheria ya Shirika la Viwango Tanzania (2009), Sheria ya Chakula na Dawa Tanzania (2003)

na Kanuni, Sheria ya Ulindaji wa Mmea (1997) na Kanuni, Sheria ya Madini (2010), Kanuni za Madini 2012, na sheria nyingine za kisekta na sheria ndogondogo za Mkoa wa Simiyu.

### *Taasisi kuu zinazohusiana na uwekezaji mkoani Simiyu na Tanzania kwa ujumla:*

Taasisi kuu zinazojishughulisha na masuala ya uwekezaji katika Mkoa wa Simiyu na Tanzania kwa ujumla ni: Kituo cha Uwekezaji Tanzania (Baruapepe: information@tic.co.tz), Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO), Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Wizara ya Biashara, Viwanda na Uwekezajira, Wakala wa Chakula na Dawa Tanzania, Mampuni ya Ugavi wa Maji katika mikoa inayohusika, Mamlaka za Manispaa katika wilaya zinazohusika (katika masuala ya ardhi), Wizara ya Maji na Umwagiliaji, na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

### *Mikakati, Mipango na Programu:*

Mikakati, mipango na programu kuu ni: Mipango ya Mwaka ya Mkoa na Taarifa za Mwaka (mf. *Taarifa ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo mwaka 2016/2017, Taarifa ya Maendeleo ya Sekta ya Mifugo Mwaka 2016/2017, etc*), Taarifa za PO-PRALG, Mipango ya Maendeleo ya Wilaya, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP II), Mkakati na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo 2017-2022 (ASDP II), Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Mifugo 2011, Ripoti za Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, na Mkakati wa Ujumuishaji wa Maendeleo ya Viwanda (IIDS 2025), Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Mpunga, Mpango wa Uwekezaji wa Kilimo na Usalama wa Chakula Tanzania, na Ukuaji wa Ushoroba wa Kilimo Tanzania.

Kwa sera hizo hapo juu, mfumo wa udhibiti, mikakati na mipango, ni wazi kuwa hali ya uwekezaji katika Mkoa wa Simiyu inaungwa mkono na mifumo ambayo inatoa mazingira yanayofaa kuhamasisha uwekezaji katika Mkoa wa Simiyu.

## 4.2 Michakato na Mahitaji

Michakato mikuu ambayo inahitajika kufanywa na mwekezaji anayetarajiwa katika Mkoa wa Simiyu imeorodheshwa hapo chini.

### *Taasisi inayoongoza:*

Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) ni wakala wa serikali ya Tanzania ulioazishwa chini ya Sheria ya Uwekezaji Tanzania Na. 26 ya 1997 kuhamasisha, kuratibu na kuwezesha uwekezaji nchini Tanzania. Kituo hiki ni mratibu kwa wawekezaji wote na kinafanya kazi za ushirikiano kwa mwekezaji tangu i maulizo mpaka kuanza kwa mradi. Kituo kinashughulikia viwanda vyote ambavyo kipato chake cha chini cha uwekezaji si chini ya Dola za Marekani 300,000 zinazomilikiwa kigeni na Dola za Kimarekani 10 0,000 zinazomilikiwa nchini. Kituo kitasaidia wawekezaji wote kupata kibali, idhini n.k., zinazotakiwa kwa mujibu wa sheria ili kuandaa na kufanya uwekezaji nchini Tanzania.

Mawasiliano ya Kituo cha Uwekezaji ni: Mkurugenzi Mtendaji, Kituo cha Uwekezaji Tanzania, Kiwanja Na; 9A&B, Mtaa wa Shabaan Robert, S.L.P 938, Dar-Es-Salaam, Tanzania, Simu: 255 22 2113365/116328-32 Faksi: 255 22 2118253, Baruapepe: tic@cats-net.com

### *Usajili:*

Usajili wa uwekezaji unaweza kufanywa katika ofisi za BRELA, katika wilaya, mkoa au taifa au katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania ambapo nyaraka zifuatazo zinahitajika: (i) Katiba ya Kampuni; (ii) Cheti cha Usajili au Cheti cha Kuandikishwa; (iii) Upembuzi yakinifu wa Uwekezaji; (iv) Cheti cha Motisha iwapo miradi imethibitishwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania; (v) Mkataba wa Ushirikiano (hati rasmi), iwapo ni ushirikiano; (vi) Mkataba wa Upangaji, (vii) Fomu ya Maombi ya Biashara (viii) Fomu za IT 21 kwa kampuni na fomu za IT 20 kwa watu binafsi, na (ix) Cheti cha Usajili wa Kampuni na Mwendeshaji cha Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN).

## *Kodi:*

Kodi zinazohusika katika miradi ya uwekezaji katika Mkoa wa Simiyu ni: (i) kodi ya mapato (30% kwa raia na wasio raia wa nchi); (ii) kodi ya Kushikilia (kwa malipo ya magawio, pensheni, bima kubwa , mirabaha, usafirishaji na mali zinazowekwa wazi); (iii) Viwango vya kodi ya mapato kwa watu binafsi (viwango vya kikomo vinaanzia 18.5% mpaka 30%); (iv) Viwango vya kodi ya mapato kwa watu binafsi ambao si raia (kiwango sawa cha 20% hutumiwa); (v) Thamani inayokatwa kodi ya mafao ya ajira (kwa ujumla mafao yote hukatwa kodi); (vi) Kodi ya mapato ya mtaji (faida/hasara wakati wa kuuza hujumuishwa katika mapato ya biashara; (vii) Ukataji kodi katika kiwango cha jumla); (viii) Ushuru wa ujuzi na maendeleo (6% ya malipo ya jumla yanayolipwa kwa wafanyakazi); (ix) Ushuru wa Mawakala wa Udhibiti kutegemea na huduma/bidhaa; na (x) Kodi ya Mamlaka ya Wilaya ambayo hutofautiana na uendeshaji na bidhaa na huduma zinazozalishwa.

Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT): VAT ni kodi ya utumiaji inayotozwa katika kiwango kimoja cha 18%. Usajili ni lazima kwa biashara yoyote, ambayo ina mapato ya zaidi ya Sh. Milioni 40 kwa mwaka. Waombaji wa usajili wa VAT wajaze fomu Na. VAT 101. Mlipakodi anatakiwa kuwasilisha mapato ya VAT ya kila mwezi katika ofisi ya karibu ya mkoa ya VAT katika siku ya mwisho ya kazi ya kila mwezi katika mwezi wa biashara.

Bidhaa za mtaji na bidhaa zinazoonekana kuwa za mtaji kwa uwekezaji hazishawishi VAT kwani VAT inatakiwa kuruhusu mwekezaji kupata unafuu wa kodi baadaye. Ulipaji wa VAT kidogokidogo katika bidhaa zozote za mtaji ni wazi kwa wafanyabiashara wote wa VAT na wasiosajiliwa.

Malipo ya VAT yanafanywa ama ndani ya siku 30 au miezi 6 kutoka tarehe rasmi kutegemeana na aina ya mlipakodi. Wafanyabiashara wanaolipa kama kawaida kama vile wasafirishaji nje wanaweza kudai malipo yao baada ya ndani ya siku 30 wakati wafanyabiashara wengine wanaweza kupata malipo yao baada ya miezi 6. Kuna bidhaa na huduma mbalimbali ambazo ama hazitozwi, kama vile usafirishaji nje au zenye msamaha wa VAT, kama vile vifaa vya tiba na huduma za utalii. Dawati la TRA katika Kituo cha Uwekezaji

litatoa orodha za bidhaa na huduma zilizo kwenye kundi hili na pia zile zenye unafuu ulioainishwa.

Kodi za mtu binafsi: Mtu ambaye ni raia na ana makazi ya kudumu nchini Tanzania anatakiwa kulipa kodi ya mapato katika mapato yake ya duniani kote. Wasio raia wanatakiwa kulipa kodi ya mapato yaliyopatikana nchini katika kiwango cha 15% cha kiasi cha jumla kilicholipwa. Mtu huyo kwa kawaida huchukuliwa kama raia iwapo ana makazi ya kudumu nchini Tanzania au alikuwa Tanzania wakati wa mwaka wa mapato kwa siku 183 au zaidi. Mtu huyo pia atachukuliwa kama raia iwapo alikuwepo katika mwaka huo wa mapato na kila mwaka kwa miaka miwili iliyofuatia ya mapato kwa kipindi cha wastani wa zaidi ya siku 122 katika kila mwaka huo wa mapato.

Mafao mengi ya mfanyakazi yanatozwa kodi. Haya yanajumuisha makazi, magari na riba - mikopo huru inayotolewa na mwajiri. Mchango kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ni 20% ya malipo ya jumla ya mfanyakazi ambapo mwajiri na mwajiriwa wote huchangia 10% kila mmoja.

Ushuru wa ujuzi na maendeleo hulipwa na muajili yeyote ambaye ameajiri watu wanne au zaidi; kiwango ni 4.5% ya ujira wa jumla. Zaidi ya hayo, ajira katika kilimo inasamehewa ushuru.

Mkoa wa Simiyu na Serikali Kuu ziko katika mchakato wa kutenganisha kodi hizi ili kuboresha muundo wa kodi, kuzifanya kuwa na uwazi zaidi, na kutowachanganya watu.

Taarifa zaidi kuhusu Kodi zinaweza kupatikana kutoka katika ofisi za Mamlaka ya Mapato Tanzania, Simu: 0800 750 075. 0800; tovuti: www.tra.go.tz, Barabara ya Edward Sokoine 28, 11105 Mchafukoge, Ilala CSR, S.L.P 11491, Dar es Salaam, Tanzania.

## 4.3 Motisha

Wawekezaji ambao wako katika sekta zinazoongoza na za kipaumbele, wanaruhusiwa msamaha wa Ushuru wa Kuingiza bidhaa na Kodi ya

Ongezeka la Thamani (*Import duty and VAT*), katika Mtaji/ Mtaji wa Bidhaa; sekta hizi ni; kilimo ikiwa ni pamoja na mifugo, Anga, Majengo ya Biashara, Biashara, Benki za maendeleo na za biashara ndogondogo, miradi inayohusiana na usafirishaji nje, maeneo Maalumu ya Maendeleo ya Kijiografia, maendeleo ya rasilimali watu, utengenezaji, Maliasili pamoja na uvuvi, mbao na ufugaji wa nyuki, ukarabati na upanuaji, utalii , utangazaji wa redio na televisheni, Usafirishaji na Miundombinu ya Uchumi. Hii inajumuisha:

***Ushuru wa Uingizaji na Msamaha wa VAT katika Bidhaa Zinazodhaniwa kuwa za Mtaji:***

Vifaa vya ujenzi, vipuri vya magari, n.k. Kulingana na mabadiliko ya bajeti ya mwaka 2013/14 msamaha wa Ushuru kwa uingizaji bidhaa unatolewa katika Bidhaa Zinazofikiriwa kuwa Mtaji kwa 75% ambapo mwekezaji atalipa 25% ya ushuru halisi wa Uingizaji. Msamaha wa VAT Unaofikiriwa kuwa Bidhaa za Mtaji ni 45% ya VAT inayolipwa, ambapo mwekezaji atalipa 55% ya VAT inayolipwa.

***Ushuru wa kuingiza (0%)*** wakati wa kuingiza nchini magari ya 4WD yaliyoundwa na kutengenezwa kwa ajili ya madhumuni ya mtalii, kulingana na vigezo vinavyotosheleza vilivyowekwa na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

***Ushuru wa kuingiza (0%)*** katika vifaa vya hotelini, ambavyo vimenakshiwa, kuchapwa, au vilivyoandikwa kwa nembo ya hoteli kwa matumizi yake.

***Unafuu Maalum wa VAT katika Bidhaa za Mtaji*** (yaanii, Bidhaa za Mtaji kwa Maelezo ya Jenasi). Huu unajumuisha: mtambo, machine, foko, winchi, vichemshaji, tanuu, vipondaji, vitia alama, matingatinga, mashine za kuchimbua, mabuldoza, *angle dozers*, lifti/ngazi za umeme n.k; vingine vyenye msamaha wa VAT ni viuavidudu, mbolea, vifaa vya tiba, mifugo bidhaa za kilimo ambazo hazijachakatwa, zana za kilimo, vitabu na magazeti, huduma za kielimu, huduma za kifedha, bidhaa za petroli, ndege, injini za ndege, sehemu za ndege, kompyuta, majenereta ya upepo na ngazi

za umeme za vimiminika, *photovoltaic* na joto la jua. Pia vinajumuishwa matanki ya upozaji wa maziwa yaliyofunikwa na majarikeni ya alumini yanayotumika kwa ajili ya kuhifadhi na kukusanya maziwa katika viwanda vinavyotoa kila siku; huduma za shambani za maandalizi ya ardhi, ulimaji, upandaji na uvunaji.

***Vikwazo vya Ushuru wa Uingizaji:*** Ushuru wa uingizaji ambao hutozwa katika pembejeo zinazoingizwa nakumika kwa ajili ya kuzalisha bidhaa kwa ajili ya kupelekwa nje na bidhaa zinazouzwa katika taasisi kama vile Umoja wa Mataifa nchini Tanzania hurudishwa.

***Utengenezaji chini ya dhamana:*** Viwanda vyote vilivyosajiliwa kutengeneza bidhaa chini ya dhamana kwa madhumuni ya usafirishaji nje vinasamehewa ushuru wa uingizaji na kodi nyingine katika zana zilizotumika kutengenezea bidhaa hizo.

***Miundombinu ya kiuchumi:*** Barabara, reli, usafiri wa anga na bahari, vifaa vya bandarini, mawasiliano ya simu, huduma za benki na bima.

***Utalii:*** Katika utalii, hasara hupelekwa mbele. Hata hivyo, kampuni zenye hasara za kudumu kwa miaka mitatu mfululizo zinatozwa 0.3% ya mapato ya mwaka. Magari ya 4WD yaliyoundwa na kutengenezwa kwa ajili ya madhumuni ya mtalii yanasamehewa ushuru wa kuingiza, kulingana na kukidhi vigezo vilivyowekwa na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vilevile, vifaa vya hotelini, ambavyo vimenakshiwa au kuchapwa au kuwekwa logo ya hoteli iliyoingizwa na hoteli yenye leseni kwa matumizi yake vinasamehewa ushuru wa kuingiza.

***Motisha kwa Wawekezaji wa Kigeni:***

Hakikisho la Uwekezaji na Utatuzi wa migogoro: Uwekezaji nchini Tanzania unahakikishwa dhidi ya utaifishaji na kunyang'anywa. Tanzania ni mwanachama wa kituo cha kimataifa kwa ajili ya Utatuzi wa Migogoro ya Uwekezaji (ICSD) na Wakala wa Hakikisho la Uwekezaji Unaohusisha nchi nyingi (MIGA).

Motisha nyingine kwa ajili ya uwekezaji wa kigeni wa moja kwa moja zinajumuisha: (i) posho ya uwekezaji inayosaidia na makato (100%) katika majengo ya kiwanda, mtambo na mashine na matumizi ya kilimo; (ii) Malipo kidogokidogo ya VAT katika mali za mtaji wa mradi; (iii) Vikwazo vya ushuru wa uingizaji; (iv) Bidhaa zinazotengenezwa za kupelekwa nje zisizo na viwango vya VAT; (v) Posho ya uchapuzi wa uchakavu wa moja kwa moja katika bidhaa za mtaji; (vi) Utambuzi wa kila mwaka wa uwekezaji wa mtaji usiopatikana katika madini; (vii) Miaka mitano ya kuendelea na hasara zote za biashara dhidi ya faida ya baadaye; (viii) kiwango cha kodi kinachofaa cha pamoja (30%) na viwango vidogo vya kodi inayoshikiliwa katika magawio (10%) na riba ya mkopo (0%); (ix) Haki ya kusafirisha nje ya nchi (100%) katika pato linaloingizwa kwa fedha za kigeni, faida na mtaji; (x) Kibali cha moja kwa moja cha kuajiri mataifa 5 ya kigeni katika mradi wenye cheti cha motisha; (xi) Ushuru wa uingizaji uliopunguzwa katika vipengele vya mtaji wa mradi; na (xii) 5% ya ushuru wa kuingiza kwa uwekezaji katika Kipaumbele.

Motisha za juu zilizotajwa kwa sasa zinapitiwa. Motisha maalumu za uwekezaji katika Mkoa wa Simiyu zinaweza kujadiliwa na kupatikana katika Menejimenti ya Mkoa wa Simiyu.

## 4.4 Ujumuishaji na ushiriki wa sekta binafsi

Ujumuishaji na ushiriki wa sekta binafsi katika mpango wa uwekezaji wa Mkoa wa Simiyu ni muhimu na unahamasishwa na Mamlaka za Mkoa wa Simiyu. Mbinu ya ushirikishaji wa sekta ya umma na binafsi unaendelezwa kuwezesha mabadiliko ya Mkoa wa Simiyu kuelekea safari ya kisasa, kibiashara na uwekezaji wa ushindani.

Kulingana na sera ya taifa ni wajibu wa Serikali kutoa viwezeshaji vya msingi kama vile ardhi, huduma za kiuchumi na kijamii (economic & social *utilities*), miundombinu, na kwa kawaida viwezeshi hujengwa kwa kutumia bajeti za Mkoa na Wilaya na Bajeti ya Taifa na rasilimali nyingine au usaidizi wa washirika wa maendeleo. Sekta binafsi ina wajibu mkubwa wa uwekeza katika Mkoa wa Simiyu, hususan katika uzalishaji, usafirishaji, uhifadhi,

uchakataji na utafutaji wa masoko ya bidhaa na kuendeleza myororo wa thamani kama ilivyo orodheshwa katika Sehemu ya 3. Hata hivyo, kwa sekta binafsi kutekeleza wajibu wake ipasavyo, mamlaka za Mkoa wa Simiyu zitaandaa mazingira wezeshi kwa kutoa miundombinu ya awali, motisha, na kuandaa au kupia upya na kusimamia utekelezaji wa sera, kanuni na taratibu nzuri za uwekezaji. Vilevile, mamlaka za mkoa zitahamasisha ushirikiano kati ya seka ya umma na binafsi, ambao ni muhimu kwa ajili ya kufikia malengo ya uhamasishaji wenye mafanikio na utekelezaji wa uwekezaji bora wa mtaji na teknolojia, kama ilivyoorodheshwa katika sehemu ya tatu ya mwongozo. Serikali ya mkoa itasimamia utozaji kodi wa haki, utoaji wa rasilimali za msingi za kutosha zinazofaa kama vile nishati, maji, mtaji wa watu wenye utaalamu, Habari na Teknolojia ya Mawasiliano, mtandao wa barabara unaofaa; na sera na kanuni imara. Vilevile, sekta binafsi lazima isaidiwe kuongeza uzalishaji na utoaji wa huduma bora ili kustawi na kuwa na ushindani kitaifa na kimataifa.

**(Footnotes)**

1 Wakati ukulima wa mikataba hasa katika pamba unaonekana kuwa na changamoto, ipo fursa ya uwekezaji hasa kwa wawekezaji katika vinu vya kuchambulia pamba na viwanda vya nguo; fursa hii itaboreka sasa ambapo serikali inarekebisha mfumo wa udhibiti wa mikataba ya ukulima ambayo italeta faida kwa wadau wote wa mzunguko wa thamani ya nguo; kutakuwa na fursa pia kwa mikataba katika kilimo cha bustani, alizeti kwa ajili ya mafuta ya kula, na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa katika sehemu nyingi za Tanzania ikiwa ni pamoja na Simiyu.

2 Katika mwaka 2010, upelekaji nje wa nguo na mavazi ya Tanzania ulifikia thamani ya jumla ya Dola za Kimarekani Milioni 140,7. Nguo za pamba (kitambaa na nyuzi) zilizalisha Dola za Kimarekani Milioni 100,4 (71%) ikifuatiwa na nguo za vitambaa za mimea (HS cat. 53) kwa Dola za Kimarekani Milioni 12,7 (9%) na kitani, kamba, kebo, nyavu (Dola za Kimarekani Milioni 9, 6 %). Upelekaji nje wa jumla ulifikia Dola za Kimarekani Milioni 11,6 ambapo Dola za Kimarekani Milioni 8.7 zilitokana na ufumaji na Dola za Kimarekani Milioni 2,9 zilijumuisha nguo za nyuzi zilizowakilisha upelekaji nje wa jumla ya 8.2 % tu.

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**
**Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Simiyu
S.L.P. 4, Bariadi.
Simu: 028 2700011 / 2700054
Barua pepe: ras.simiyu@tamisemi.go.tz
Tovuti: www.simiyu.go.tz

ISBN: 978 - 9987 - 770 - 28 - 1